**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

National Development Plan | Strategy and Plans Development Books

2014

# Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2013-2014

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/754

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2013/14

**OFISI YA RAIS,**
**TUME YA MIPANGO**

**MACHI, 2013**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

--------------

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2013/14

**OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO**

**MACHI, 2013**

# YALIYOMO


**UTANGULIZI** .................... iv

**SURA YA KWANZA** .................... 1

**HALI YA UCHUMI** .................... 1

1.1 Utangulizi .................... 1

1.2 Hali ya Uchumi wa Dunia .................... 1

1.3 Ukuaji wa Pato la Taifa .................... 2

1.4 Mfumuko wa Bei .................... 2

1.5 Ujazi wa Fedha na Karadha .................... 3

1.6 Mikopo kwa Sekta Binafsi .................... 3

1.7 Mwenendo wa Viwango vya Riba .................... 4

1.8 Sekta ya Nje .................... 4

1.9 Thamani ya Shilingi .................... 5

1.10 Akiba ya Fedha za Kigeni .................... 5

1.11 Deni la Taifa .................... 6

1.12 Mapato na Matumizi ya Serikali .................... 6

1.13 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla .................... 7

**SURA YA PILI** .................... 9

**UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA NUSU MWAKA 2012/13 MWAKA 2012/13** .................... 9

2.1 Utangulizi .................... 9

2.2 Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kwa nusu ya kwanza 2012/13 .................... 9

2.3 Maeneo ya Kipaumbele ya Kimkakati .................... 9

2.3.1 Miundombinu .................... 9

2.3.2 Kilimo .................... 17

2.3.3 Viwanda .................... 19

2.3.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu .................... 20

2.3.5 Huduma za Utalii na Fedha .................... 20

2.3.6 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa .................... 21

2.4 Maeneo Mengine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi .................... 21

2.4.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundi ........................................21
2.4.2 Afya na Ustawi wa Jamii ........................................23
2.4.3 Mifugo na Uvuvi ........................................23
2.4.4 Madini ........................................25
2.4.5 Usafiri wa Anga ........................................25
2.4.6 Hali ya Hewa ........................................26
2.4.7 Maendeleo ya Teknolojia na Ubunifu ........................................26
2.4.8 Ardhi, Nyumba na Makazi ........................................27
2.4.9 Utawala Bora ........................................27
2.4.10 Katiba Mpya ........................................27
2.4.11 Utambulisho wa Kitaifa ........................................27
2.4.12 Sensa ya Watu na Makazi 2012 ........................................28
2.4.13 Mchango wa Sekta Binafsi ........................................28
2.5 Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa ........................................28

**SURA YA TATU** ........................................30
**MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2013/14** ........................................30
3.1 Utangulizi ........................................30
3.2 Vigezo vya Kuainisha Miradi ya Kipaumbele ya Kimkakati ........................................30
3.3 Maeneo ya Kimkakati kwa mwaka 2013/14 ........................................30
3.3.1 Miundombinu ........................................30
3.3.2 Kilimo ........................................31
3.3.3 Viwanda ........................................32
3.3.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu ........................................32
3.3.5 Utalii na Huduma za Fedha ........................................32
3.3.6 Huduma za kifedha ........................................32
3.4 Maeneo Mengine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi ........................................32
3.4.1 Elimu / Mafunzo ya Ufundi ........................................33
3.4.2 Afya na Ustawi wa Jamii ........................................33
3.4.3 Mifugo na Uvuvi ........................................33
3.4.4 Misitu na Wanyamapori ........................................33
3.4.5 Madini ........................................33
3.4.6 Ardhi, Nyumba na Makazi ........................................34

3.4.7 Usafiri wa Anga ........ 34
3.4.8 Hali ya Hewa ........ 34
3.4.9 Biashara na Masoko ........ 34
3.4.10 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ........ 34
3.4.11 Utambulisho wa Kitaifa ........ 35
3.4.12 Utawala Bora ........ 35
3.4.13 Katiba Mpya ........ 35
3.4.14 Kazi na Ajira ........ 35

**SURA YA NNE** ........ 36
**UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA** ........ 36
4.0 Utangulizi ........ 36
4.1 Gharama za Kutekeleza Mpango ........ 36
4.2 Vyanzo vya Mapato ya Ndani ........ 36
4.3 Vyanzo vya Mapato ya Nje ........ 36
4.4 Kukuza Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ........ 36
4.5 Kuvutia Uwekezaji wa Sekta Binafsi ........ 37

**SURA YA TANO** ........ 38
**UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MPANGO** ........ 38
5.0 Utangulizi ........ 38
5.1 Mpangilio wa Utekelezaji ........ 38
5.2 Ufuatiliaji na Tathmini ........ 38
5.3 Utaratibu wa Kusimamia Fedha za Maendeleo ........ 39
5.4 Mfumo wa Kusimamia Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini kwa Miradi ya Maendeleo ........ 40
5.5 Muhtasari wa Uratibu wa Utekelezaji ........ 40

# UTANGULIZI

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/14 ni ya pili katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, mapendekezo hayo yanajikita katika kuendelea kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano vifuatavyo: (i) Miundombinu ya nishati, usafirishaji, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), maji safi na maji taka na umwagiliaji; (ii) Kilimo ikijumuisha mazao ya chakula na biashara, malighafi ya viwandani, ufugaji, uvuvi na misitu; (iii) Viwanda vinavyotumia malighafi hususan za ndani na kuongeza thamani, viwanda vikubwa vya mbolea na saruji, viwanda vya kanda maalum za kiuchumi, kielektroniki na TEHAMA; (iv) Maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi kwa kutilia mkazo sayansi, teknolojia na ubunifu na kuimarisha mafanikio ya upatikanaji wa huduma za jamii; na (v) Uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

Mapendekezo ya mwaka 2013/14 hayatofautiani sana na maeneo yaliyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2012/13. Kimsingi Mpango wa Mwaka 2013/14 ni wa kuimarisha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2012/13. Katika maeneo muhimu ya mapendekezo haya ambayo ni vipaumbele vya kimkakati Serikali itaendelea kujikita katika kuwezesha sekta binafsi kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/14 unabainisha misingi, malengo, vipaumbele, mikakati ya utekelezaji, na changamoto zilizopo hivi sasa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Lengo kuu la mapendekezo haya ni kuongoza utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo ambao Serikali inakusudia kuutekeleza katika mwaka 2013/14 utakaozingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010; Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini - MKUKUTA (2011-2015), vipaumbele vya kisekta na Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2013/14.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/14 yamepangiliwa katika sura kuu tano. Sura ya kwanza inaeleza mwenendo wa uchumi kwa kipindi cha mwaka 2011/12 na nusu ya kwanza ya 2012/13. Pia sura hii inabainisha shabaha na malengo yanayotarajiwa kufikiwa katika kipindi cha mwaka 2013/14. Sura ya pili ni mapitio ya utekelezaji katika maeneo ya kipaumbele ya kimkakati na mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha nusu mwaka 2012/13. Aidha, katika baadhi ya maeneo mapitio ya utekelezaji yameanishwa kwa kipindi cha robo mwaka 2012/13 kutegemea upatikanaji wa taarifa na takwimu husika. Sura ya tatu, ndiyo kiini cha Mpango na inabainisha maeneo yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/14. Sura ya nne ni mapendekezo ya namna ya kugharamia Mpango; na sura ya tano inaainisha mfumo wa utekelezaji, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango.

# SURA YA KWANZA

# HALI YA UCHUMI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mwenendo wa uchumi wa Dunia, ukuaji wa Pato la Taifa, mfumuko wa bei, ujazi wa fedha na karadha, mikopo kwa sekta binafsi, mwenendo wa viwango vya riba, sekta ya nje, thamani ya shilingi, akiba ya fedha za kigeni, deni la taifa, mapato na matumizi ya Serikali na shabaha na misingi ya uchumi jumla.

## 1.2 Hali ya Uchumi wa Dunia

Mwenendo wa uchumi wa Dunia unaonyesha ukuaji unaopungua katika kipindi kijacho kulingana na Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF, Oktoba 2012). Pato la dunia linatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.3 kwa mwaka 2012 kutoka asilimia 3.8 mwaka 2011. Kushuka kwa ukuaji kunatokana na kudhoofika kwa shughuli za kiuchumi na biashara ya kifedha katika nchi za Ulaya kulikosababishwa na mgogoro wa madeni (Euro Debt Crisis), hususan katika nchi za Ugiriki na Hispania. Ukuaji kwa Nchi Zinazoibukia Kimaendeleo na Zinazoendelea linakisiwa kuwa asilimia 5.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 6.2 mwaka 2011. Kwa upande wa Nchi za Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika, ukuaji wa pato unaonesha kuimarika zaidi mwaka 2012 na 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa mwaka 2011. Hii inatokana na kuimarika kwa uzalishaji wa mafuta hasa baada ya nchi ya Libya kuanza uzalishaji kwa kasi baada ya kipindi cha vurugu mwaka 2011.

Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ni wa kuridhisha licha ya changamoto za mgogoro wa madeni katika nchi za Ulaya. Ukuaji kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaonesha taswira inayotofautiana kwa baadhi ya nchi kuwa na viwango vya ukuaji unaongezeka na nchi nyingine kushuka. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Rwanda na Uganda zinatarajiwa kupungua wakati zile zilizosalia ukuaji wake unatarajiwa kuongezeka. Jedwali Na.1 linaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Dunia na matarajio kwa kipindi cha mwaka 2006 hadi 2013.

**Jedwali Na. 1: Ukuaji Pato la Dunia na Matarajio 2006 hadi 2013 (Asilimia)**


| | Halisi | | | | | | Matarajio | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2006 | 2007 | 2008 | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
| Dunia | 5.3 | 5.4 | 2.8 | -0.7 | 5.1 | 3.8 | 3.3 | 3.6 |
| Nchi Zilizoendelea | 3.1 | 2.8 | 0.1 | -3.7 | 3.0 | 1.6 | 1.3 | 1.5 |
| Nchi Zinazoibukia Kimaendeleo na Zinazoendelea | 8.2 | 8.9 | 6.0 | 2.8 | 7.4 | 6.2 | 5.3 | 5.6 |
| Nchi Zinazoibukia Barani Asia | 10.3 | 11.5 | 7.7 | 7.2 | 9.5 | 7.8 | 6.7 | 7.2 |
| Nchi za Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika | 6.3 | 5.7 | 4.5 | 2.6 | 5.0 | 3.3 | 5.3 | 5.6 |
| Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara | 6.4 | 7.1 | 5.6 | 2.8 | 5.3 | 5.1 | 5.0 | 5.7 |
| Burundi | 5.4 | 4.8 | 5.0 | 3.5 | 3.8 | 4.2 | 4.2 | 4.5 |
| Kenya | 6.3 | 7.0 | 1.5 | 2.7 | 5.8 | 4.4 | 5.1 | 5.6 |
| Rwanda | 9.2 | 5.5 | 11.2 | 4.1 | 7.2 | 8.6 | 7.7 | 7.5 |
| Uganda | 9.5 | 8.6 | 7.7 | 7.0 | 6.1 | 5.1 | 4.2 | 5.7 |
| Tanzania | 6.7 | 7.1 | 7.4 | 6.0 | 7.0 | 6.4 | 6.8 | 7.0 |

**Chanzo**: Shirika la Fedha la Kimataifa, 2012

## 1.3 Ukuaji wa Pato la Taifa

Pamoja na matarajio ya hali ya uchumi wa Dunia kuonesha kuwa kasi ya ukuaji inatarajiwa kupungua, uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara licha ya changamoto za ukosefu wa umeme wa uhakika. Katika kipindi cha mwaka 2012, kiwango halisi cha ukuaji wa uchumi kilikuwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2011. Thamani halisi ya Pato la Taifa (GDP) kwa mwaka 2012 ni shilingi 44,717,663 milioni ikilinganishwa na shilingi 37,532,962 milioni mwaka 2011. Mchango mkubwa wa kiuchumi ulitokana na shughuli za Huduma kwa asilimia 47.6, kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uwindaji) kwa asilimia 26.8, Viwanda na Ujenzi asilimia 24.0 na Uvuvi asilimia 1.6.

**Mchoro Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa mwaka 2001 - 2012**




**Chanzo**:Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2012

## 1.4 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei umepungua kutoka wastani wa asilimia 19.8 Disemba, 2011 hadi kufikia asilimia 12.1 Disemba 2012 kutokana hasa na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia hususan katika nusu ya kwanza ya mwaka 2012. Wastani wa mfumuko wa bei wa chakula umeshuka kufikia asilimia 13.3 Disemba 2012 kutoka asilimia 25.6 Disemba 2011 kutokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika ukanda wa Afrika Mashariki. Aidha, mfumuko wa bei wa nishati ulishuka kufikia asilimia 17.8 kutoka asilimia 41.0 katika kipindi hicho kufuatia juhudi za serikali za kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme. Jedwali Na.2, linaonesha mwenendo wa kasi ya upandaji bei katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2012 kwa makundi tofauti ya bidhaa na huduma.

**Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Makundi Januari, 2012 hadi Februari, 2013**

| Mfumuko wa Bei | Jan-12 | Feb-12 | Mar-12 | Apr-12 | May-12 | Jun-12 | Jul-12 | Aug-12 | Sep-12 | Oct-12 | Nov-12 | Dec-12 | Jan-13 | Feb-13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chakula | 26.2 | 25.5 | 24.9 | 24.7 | 24.5 | 22.9 | 20.3 | 18.5 | 15.8 | 15.0 | 13.7 | 13.3 | 12.1 | 11.7 |
| Nishati | 30.1 | 33.5 | 29.4 | 24.9 | 21.2 | 20.5 | 16.3 | 16.9 | 19.4 | 18.4 | 17.8 | 21.7 | 17.4 | 18.3 |
| Bidhaa na huduma zote za jamii chakula na vinywaji baridi | 11.8 | 11.8 | 11.5 | 11.2 | 10.5 | 10.5 | 10.0 | 10.3 | 10.5 | 10.1 | 10.3 | 10.7 | 9.3 | 8.4 |
| Huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 9.0 | 8.6 | 8.8 | 9.0 | 8.7 | 8.8 | 8.8 | 9.2 | 8.9 | 8.6 | 8.9 | 8.8 | 7.9 | 6.7 |
| **Mfumuko wa Bei -Overall** | **19.7** | **19.4** | **19.0** | **18.7** | **18.2** | **17.4** | **15.7** | **14.9** | **13.5** | **12.9** | **12.7** | **12.1** | **10.9** | **10.4** |

Chanzo: NBS, 2013

Hadi Februari, 2013 mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 10.4 ikilinganishwa na asilimia 19.4 Februari, 2012. Kushuka kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na kupungua kwa bei ya bidhaa zisizo za vyakula. Mfumuko wa bei ya bidhaa zisizo za vyakula umepungua kutoka asilimia 9.3 Januari, 2013 hadi asilimia 8.4 mwezi Februari, 2013. Mfumuko wa bei kwa bidhaa za vyakula umepungua hadi asilimia 11.7 mwezi wa Februari, 2013 ikilinganishwa asilimia 12.1 mwezi wa Januari, 2013.

Mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi jirani na Tanzania hasa zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni wa kuridhisha ikizingatiwa kuwa viwango vya upandaji bei viko chini ya tarakimu moja (single digit level) kutoka kiwango cha zaidi ya asilimia 18 Januari 2012. Kasi ya upandaji bei kwa nchi ya Uganda na Kenya ilifikia asilimia 3.4 na 4.4 Februari, 2013 ikilinganishwa na asilimia 4.9 na 3.6 Januari, 2013 kwa mtiririko huo.

## 1.5 Ujazi wa Fedha na Karadha

Katika mwaka 2012/13, sera ya fedha ililenga kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)[1] lisilozidi asilimia 17.4. Aidha, kiwango hicho cha ukuaji wa ujazi wa fedha kinaendana sambamba na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 20.0. Katika mwaka ulioishia Novemba, 2012, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulikua kwa kiwango cha asilimia 11.1 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 21.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba, 2011, kiwango ambacho ni cha chini ikilinganishwa na lengo la asilimia 17.4 kwa mwaka unaoishia Juni, 2013. Kasi ya chini ya ongezeko la ujazi wa fedha ilitokana na kupungua kwa rasilimali halisi za nje

1 *M3 = M2 + Amana za fedha za kigeni*
*M2 = M1 + Amana za muda maalumu + Amana za akiba*
*M1 = Fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabenki + Amana za hundi*

(Net foreign assets) katika mfumo wa mabenki ambapo jumla ya shilingi bilioni 195.8 zilipungua kwa mwaka unaoishia Novemba 2012 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 492.0 mwaka unaoishia Novemba 2011. Aidha, kiwango cha kuongezeka kwa rasilimali halisi za ndani (Net domestic assets) kilipungua na kuwa na ongezeko la shilingi bilioni 1,663.6 mwaka unaoishia Novemba 2012 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 1,809.0 mwaka unaoishia Novemba 2011.

## 1.6 Mikopo kwa Sekta Binafsi

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 18.7 katika kipindi kilichoishia Juni 2012 ikilinganishwa na lengo la asilimia 23.0 katika kipindi hicho. Shughuli nyingi za kiuchumi zilikuwa na viwango vidogo vya ukuaji isipokuwa ujenzi. Mikopo mingi ilielekezwa katika shughuli za biashara ambayo ilikuwa ni asilimia 21.4 ya mikopo yote iliyoelekezwa kwa sekta binafsi. Hii ilifuatiwa na mikopo kwa shughuli binafsi ambazo zilikuwa ni asilimia 21.3, uzalishaji viwandani asilimia 10.9 na kilimo asilimia 10.6. Hadi Oktoba 2012, mikopo kwa sekta binafsi ilifikia shilingi bilioni 8,866.5. Uwiano wa shughuli za kiuchumi ulionyesha kuwa mikopo kwa ajili ya shughuli za kibiashara ilichangia asilimia 20.6 ya mikopo yote kwa sekta binafsi, shughuli binafsi (asilimia 20.3), kilimo (asilimia 11.8) na uzalishaji viwandani (asilimia 11.5).

## 1.7 Mwenendo wa Viwango vya Riba

Viwango vya riba vinavyotozwa katika huduma mbalimbali za kibenki vimeonekana kuwa na sura mchanganyiko. Pengo kati ya riba za mikopo na zile za akiba limepungua kwa kiasi hasa kwa mikopo ya mwaka mmoja na ile ya muda mfupi. Wastani wa jumla wa viwango vya riba za amana za muda maalum kwenye mabenki uliongezeka hadi asilimia 8.40 mwezi Novemba 2012 kutoka asilimia 6.73 mwezi Novemba 2011. Kiwango cha riba za amana za muda mfupi (miezi 12) kiliongezeka kutoka asilimia 8.05 Novemba 2011 hadi asilimia 9.36 katika kipindi kilichoishia Novemba 2012. Aidha, kiwango cha riba za mikopo (mwaka mmoja) kiliongezeka hadi asilimia 14.46 katika kipindi kilichoishia Novemba 2012 kutoka asilimia 13.53 mwezi Novemba 2011. Kufuatia mwenendo huu, tofauti kati ya riba za mikopo (mwaka mmoja) na zile za amana za muda mfupi ilipungua kufikia asilimia 5.10 mwezi Novemba 2012 kutoka asilimia 5.48 mwezi Novemba 2011.

Mwenendo huu wa riba bado si wa kuridhisha hasa katika kuvutia uwekezaji na uanzishwaji wa biashara katika uchumi. Hatua za kuongeza kasi ya

mageuzi katika sekta ya fedha inapaswa kuimarishwa. Miongoni mwa hatua hizo ni kuongeza juhudi katika utekelezaji wa mfumo wa taarifa kwa ajili ya wakopaji (credit reference databank system), kuimarisha mfumo wa usimamizi katika *Saving and Credit Cooperative Society* (SACCOS); na kuanzisha sera kwa ajili ya wakopaji wadogo.

## 1.8 Sekta ya Nje

Hadi kufikia Novemba, 2012, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 7,811.5 ni sawa na ongezeko la asilimia 16.4, ikilinganishwa na thamani ya mauzo nje kwa kipindi kama hicho mwaka 2011. Ongezeko hilo lilitokana na mauzo ya bidhaa za asilia na zisizo za asilia, ambapo mauzo ya bidhaa za asilia yaliongezeka kwa asilimia 37.4 hadi Dola milioni 816.9, na zile zisizo za asilia iliongezeka kwa asilimia 12.8 na kufikia Dola milioni 3,863.1. Vilevile, thamani ya biashara ya huduma ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 2,429.5 Novemba 2012 ikilinganishwa na Dola milioni 2,089.6 Novemba, 2011, sawa na ongezeko la asilimia 16.3


Thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma katika mwaka ulioishia Novemba 2012 ilifikia Dola za Kimarekani milioni 11,609.1 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.1, ikilinganishwa na thamani ya uagizaji kipindi kama hicho mwaka 2011. Katika kipindi hicho, bidhaa za ukuzaji mitaji ziliongezeka hadi Dola za Kimarekani milioni 3,399.9, sawa na ongezeko la asilimia 8.9. Aidha, uagizaji wa bidhaa kwa ajili ya malighafi ya viwanda uliongezeka hadi Dola milioni 3,941.5, sawa na ongezeko la asilimia 9.0. Bidhaa za kawaida ikijumuisha chakula, thamani yake iliongezeka hadi Dola za Kimarekani milioni 2,126.6, sawa na ongezeko la asilimia 10.6. Thamani ya huduma kutoka nje ilifikia Dola za Kimarekani milioni 2,139.0 katika mwaka unaoishia Novemba 2012 ikilinganishwa na Dola milioni 1,975.3, sawa na ongezeko la asilimia 8.3 katika kipindi kama hicho 2011.

Mwenendo wa biashara ya nje unaonyesha kuwa, urari wa biashara ya nje ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 3,314.4 kufikia Novemba 2012, ikilinganishwa na Dola milioni 3,524.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2011. Kupungua huko kwa nakisi ya urari wa biashara kulitokana na ongezeko kubwa la mauzo nje ikilinganishwa na uagizaji toka nje.

## 1.9 Thamani ya Shilingi

Thamani ya shilingi ya Tanzania kwa Dola ya Kimarekani ilikuwa ya wastani wa shilingi 1,572.2 kwa Dola kati ya kipindi cha Januari hadi Juni 2012.

Kiwango cha chini kabisa katika kipindi hicho kilikuwa shilingi 1,565.0 kwa dola na kiwango cha juu kilikuwa shilingi 1,581.4 kwa dola. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani kunatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya dola kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma hasa mafuta. Hadi Oktoba 2012, thamani ya shilingi ya Tanzania ilifikia shilingi 1,572.0 kwa dola moja ya kimarekani sawa na kuongezeka kwa thamani ya shilingi kwa asilimia 5.0 kutoka shilingi 1,646.4 Oktoba 2011.




**Chanzo**: Benki Kuu ya Tanzania, 2012

## 1.10 Akiba ya Fedha za Kigeni

Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kimeendelea kuwa cha kuridhisha, ambapo hadi Novemba, 2012 kilikuwa Dola za Kimarekani milioni 3,883.6 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 3,764.9 kwa mwezi Novemba 2011. Kiasi hiki ni sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa muda wa miezi 4.0 ikilinganishwa na lengo la miezi 4.5 hadi Juni 2013. Kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni kumetokana na uingiaji wa fedha za kigeni kama vile misaada ya maendeleo, uwekezaji wa moja kwa moja toka nje na mikopo kutoka nje. Hata hivyo, kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni hakijumuishi fedha za kigeni zinazomilikiwa na mabenki ya biashara zenye jumla ya Dola za Kimarekani milioni 884.1.

## 1.11 Deni la Taifa

Deni la Taifa ambalo linajumuisha deni la Umma na Sekta binafsi, limeongezeka kufikia dola za kimarekani bilioni 12.687 Juni 2012 kutoka dola za kimarekani bilioni 11.51 Juni 2011. Kati ya hilo, deni la umma lilikuwa dola za kimarekani bilioni 10.8. Deni la nje katika kipindi kilichoishia Juni 2012 lilifikia dola za kimarekani bilioni 10.1 (kati ya hilo, dola bilioni 8.2

zikiwa ni deni la nje la Serikali) ikilinganishwa na dola za kimarekani bilioni 8.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2011. Deni la ndani katika kipindi hicho lilikuwa dola za kimarekani bilioni 2.6. Aidha, katika kipindi kilichoishia Juni 2012, malipo ya deni la Serikali yalikuwa shillingi bilioni 516.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 396.3 Juni 2011. Kati ya kiasi hicho, malipo ya deni la nje yalikuwa shilingi bilioni 171.7 wakati ambapo malipo ya deni la ndani yalikuwa shilingi bilioni 345.1.

Hadi Septemba 2012, Deni la Taifa likijumuisha deni la Serikali na Sekta binafsi, lilifikia Dola za Kimarekani milioni 12,817.6 ikilinganishwa na Dola milioni 9,722.9 mwishoni mwa Septemba 2011. Kati ya kiasi hicho, Dola za Kimarekani milioni 11,384 ni deni la Serikali na Dola za Kimarekani milioni 1,433.6 ni deni la Sekta binafsi. Deni la nje la Serikali lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 7,964.5 wakati deni la ndani lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 3,419.5. Ongezeko hilo limetokana hasa na mikopo mipya yenye masharti nafuu na kibiashara na malimbikizo ya riba ya deni la nje hasa kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ambazo hazijatoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano.

Katika kutekeleza mkakati wa taifa wa madeni, Serikali imeendelea kusimamia mikopo kwa karibu hasa kwa kuhakikisha kuwa inakopa kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu (concessional loans) kwa ajili ya kugharamia uendelezaji wa miundombinu. Hata hivyo, kwa kuzingatia changamoto za miundombinu zilizopo kwa sasa, hasa katika nishati, reli, barabara na bandari, Serikali katika kipindi cha mwaka 2010/11 ilianza kukopa mikopo ya kibiashara (non-concessional loans) ili kukidhi mahitaji ya kuendeleza miundombinu. Tathmini iliyofanyika Februari 2012 inaonesha kuwa deni la Taifa bado linahimilika japokuwa hali ya uhimilivu inazidi kupungua ikilinganishwa na tathmini kama hiyo iliyofanyika Oktoba 2010. Hii inamaanisha kuwa kuna haja ya kutumia mikopo ya kibiashara kwa tahadhari na umakini mkubwa.

### 1.12 Mapato na Matumizi ya Serikali

Mwaka 2011/12, jumla ya makusanyo ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 7,220.9 sawa na asilimia 101 ya makadirio kwa kipindi hicho na ongezeko la asilimia 22 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2010/11. Aidha, mapato yanayotokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 6,480.5 ikiwa ni asilimia nne zaidi ya makadirio kwa kipindi hicho, kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa makusanyo na hatua za kisera zilizochukuliwa na Serikali. Mapato yasiyo ya kodi katika kipindi hicho yalikuwa shilingi bilioni 545.4, sawa na asilimia 97 ya

makadirio kwa kipindi husika. Katika kipindi cha mwaka 2011/12, jumla ya matumizi yalikuwa asilimia 86 ya makadirio ya bajeti. Matumizi ya kawaida yalipunguzwa ili kuendana na upatikanaji wa fedha. Pamoja na kwamba matumizi ya maendeleo yalikuwa chini ya lengo, fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo zilitolewa kama ilivyopangwa.

Utekelezaji wa bajeti kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2012/13 ulikuwa wa kuridhisha. Jumla ya Mapato yote kutoka vyanzo vya Kodi na visivyo vya kodi ilifikia shilingi bilioni 4,302.1 sawa na asilimia 93 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 4,618.7 ya mapato yote kwa mwaka. Kwa upande mwingine matumizi yalifikia shilingi bilioni 7,236.7 ikiwa ni sawa na makadirio ya shilingi bilioni 7,554.8 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5,346.1 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1,890.6 ni matumizi ya maendeleo.

## 1.13 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla

**Shabaha**

Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha 2013/14- 2015/16 ni kama ifuatavyo:-

a) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.8 mwaka 2012, asilimia 7.0 mwaka 2013, asilimia 7.5 mwaka 2014, asilimia 8.0 mwaka 2015 na asilimia 8.5 mwaka 2016;

b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja katika kipindi cha muda wa kati;

c) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka asilimia 17.4 ya Pato la Taifa mwaka 2011/12 kufikia asilimia 18.2 ya Pato la Taifa mwaka 2012/13, na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 18.7 mwaka 2015/16;

d) Kuongeza mapato yatokanayo na kodi kutoka asilimia 15.7 ya Pato la Taifa mwaka 2011/12 hadi asilimia 16.6 mwaka 2012/13 na asilimia 18.1 ifikapo mwaka 2015/16;

e) Kupunguza kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kufikia asilimia 17.4 mwaka 2012/13 na kuibakisha katika kiwango cha asilimia 15 katika kipindi cha muda wa kati sambamba na lengo la kupunguza mfumuko wa kasi ya upandaji bei;

f) Kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 20.0 ya Pato la Taifa Juni 2013;

g) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) hadi kufikia asilimia 5.5 au chini zaidi katika kipindi cha muda wa kati; na

h) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya

uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

**Misingi**

Misingi ya Mpango kwa kipindi cha 2013/14 ni kama ifuatavyo:

a) Kuendelea kuimarisha utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii;
b) Kuwepo kwa nishati ya umeme wa uhakika;
c) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
d) Kuendelea kuimarika kwa thamani ya shilingi;
e) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;
f) Kuimarisha utekelezaji wa Sera za Fedha na Bajeti;
g) Kuendelea kuimarika kwa mahusiano na Washirika wa Maendeleo;
h) Kuendelea kutekeleza sera ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi;
i) Kuendelea na utekelezaji wa maboresho katika sekta ya umma;
j) Kuboresha zaidi mazingira kwa ajili ya kuvutia biashara na kuongeza tija;
k) Kupunguza utegemezi; na
l) Kuimarisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo.

# SURA YA PILI

# UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA NUSU MWAKA 2012/13

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mafanikio na changamoto zilizojitokeza kwa nusu mwaka katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2012/13 katika maeneo ya kipaumbele, pamoja na maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

## 2.2 Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kwa nusu ya kwanza 2012/13

Katika bajeti ya mwaka 2012/13, Serikali ilikadiria kutumia fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 2,028.9 na fedha za nje kiasi cha shilingi bilioni 1,995 kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Desemba 2012, jumla ya matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,004.9 sawa na asilimia 88.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 2,263.9. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 949.2, sawa na asilimia 86 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,106.8 na fedha za nje zilifika shilingi bilioni 1,055.6 sawa na asilimia 91 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,157.1. Kati ya fedha za ndani Wizara, Idara zinazojitegemea na Taasisi zilipewa jumla ya shilingi bilioni 770.7, Sekretarieti za Mikoa zilipewa shilingi bilioni 16.4 na Halmashauri zote nchini zilipewa jumla ya shilingi bilioni 162.2.

### 2.3.1 Miundombinu

### A. Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji

**a) Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini, Dar es Salaam**

Katika mwaka 2012/13, Serikali imetenga shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi walio kwenye eneo la uwekezaji Kurasini. Hatua iliyofikiwa ni kuanza kwa zoezi la tathmini ya fidia ambalo linatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Aprili, 2013. Mwekezaji YIWU-Panafrica International Investment Corporation kutoka China ameonesha nia ya kuwekeza katika Kituo cha Kurasini kwa Dola za Kimarekeni milioni 400 sawa na shilingi bilioni 640.

## b) Reli

### i) Reli ya Kati

Katika mwaka wa fedha 2012/13, reli ya kati imetengewa shilingi bilioni 24.7 kwa ajili ya ukarabati wa Kilomita 89 kwa 80lb/yards kati ya km 197 pamoja na ununuzi wa vifaa na mataruma; ukarabati na uboreshaji wa njia ya reli eneo la Kidete – Gulwe; Ujenzi wa daraja katika eneo la Bahi- Kintinku na madaraja yaliyoko km 293 na km 303 kutoka Dar es Salaam; ukarabati wa injini na mabehewa, magenge; na ukarabati wa njia kuu. Utekelezaji ni kama ifuatavyo:

i. Mradi wa kutandika reli yenye uzito wa ratili 80 kwa yadi unaotekelezwa na Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* (CCECC) kati ya Stesheni ya Malongwe na Kitaraka (km 89) unaendelea. Mradi huu ulianza Septemba 2012 na unatarajiwa kuchukua miezi 12 kwa gharama ya shilingi bilioni 29.2. Shehena ya reli 3,120 zinazoweza kutandika km 32 na mataruma 3,678 zimekwisha safirishwa na kuwasili eneo la kazi;
ii. Matengenezo katika maeneo 32 yaliyopo kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe yaliyokuwa yameharibiwa na mvua yamekamilika. Aidha, maeneo mapya ya kati ya stesheni ya Godegode na Gulwe yamefanyiwa matengenezo;
iii. Ujenzi wa madaraja 3 (km 239, km 303 na km 517 kutoka Dar es Salaam) umeanza ambapo njia ya mchepuo katika daraja la Kintinku (km 517) iii kuruhusu ujenzi ulikamilika na kutumika. Ujenzi ulianza Juni, 2012 na unatarajiwa kuchukua miezi 16 kwa gharama ya shilingi bilioni 14.45 unaofanywa na Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* (CCECC) ya China; na
iv. Ukarabati wa injini na mabehewa ya treni unaendelea ambapo injini 2 kati ya 4 za njia kuu zimekamilika na zinatumika, injini 2 za usafiri wa abiria jijini Dar es Salaam zimekamilika na zinatumika. Ukarabati wa mabehewa 15 kati ya 82 ya mizigo na 21 kati ya 31 ya abiria umekamilika. Aidha, ununuzi wa injini mpya 13, kazi ya kujenga upya injini 8 za njia kuu, kukarabati injini za njia kuu, ukarabati na ununuzi wa mabehewa mapya na vifaa vya uokoaji vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

### ii) Reli ya Tanga (Mwambani) – Arusha – Musoma

Katika mwaka 2012/13, kazi iliyopangwa kufanyika katika mradi huu ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina (kuandaa michoro na gharama za mradi). Taratibu za kumpata mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika.

**iii) Reli ya Kikanda**

Reli ya Dar es Salaam – Isaka –Kigali- Keza/Geita-Msongati (km 1,464). Katika mwaka 2012/13, fedha zimetengwa kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa reli hii. Kazi ya upembuzi yakinifu kupitia Kampuni ya *Canadian Rail* (CANARAIL) ya Canada umekamilika. Taarifa ya maendeleo ya kazi (Interim report) imeshawasilishwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali.

**iv) Mafanikio Mengine**

Katika kupunguza adha ya usafiri jijini Dar es Salaam, usafiri wa treni ya abiria (Ubungo-Stesheni, Tabata-Stesheni na Pugu Mwakanga-TAZARA) umeanzishwa mwezi Novemba, 2012. Utaratibu wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupandia abiria na maegesho ya magari unaendelea.

**c) Bandari**

**i. Bandari ya Dar es Salaam.**

Katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuimarisha na kuongeza kina cha maji katika gati nambari moja hadi nambari saba za bandari ya Dar es salaam. Mradi una lengo la kuongeza kina cha gati hadi mita 12 na kuongeza uwezo wa kuhifadhi mizigo. Mradi huu unatekelezwa na Mamlaka ya Bandari kwa kushirikiana na *Trade Mark East Africa* (TMEA), Benki ya Maendeleo ya kusini mwa Afrika (*Development Bank of South Africa* – DBSA) na kusimamiwa na mtaalam mwelekezi, Kampuni ya Inros Lackner AG ya Ujerumani. Utekelezaji ni: upembuzi yakinifu wa mradi huu ulianza mwezi Mei, 2012 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Machi, 2013.

**ii. Kituo cha Uchukuzi wa Mizigo Kisarawe, Pwani**

Katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu Kisarawe. Awamu ya kwanza ya upembuzi yakinifu ilikamilika mwaka 2010 chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Mchakato wa zabuni za kumpata Mtalaam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu awamu ya pili (Study & Detailed Engineering Designs) unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Machi 2013. Mwezi Desemba 2012 Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe ilitenga eneo lenye ukubwa wa Ekari 1,468 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari kavu. Kazi ya kufanya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia inatarajia kukamilika mwezi Aprili 2013.

### iii. Bandari ya Mwambani Tanga

Katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mwambani Tanga. Utekelezaji ni: Kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga bandari mpya ya Mwambani – Tanga ulikamilika mwezi Disemba, 2012. Mamlaka ya Bandari kwa kushirikiana na Serikali inaendelea na hatua za kutafuta wawekezaji na fedha za kuendeleza mradi.

### iv. Bandari ya Mtwara

Katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya upanuzi na uboreshaji wa bandari ya Mtwara. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu Oktoba, 2012. Pamoja na mapendekezo mengine, taarifa ya upembuzi yakinifu imependekeza upanuzi wa bandari ya Mtwara ufanyike katika awamu mbili: ujenzi wa gati nne na kuanzishwa kwa eneo huru (Freeport zone) kwa ajili ya kuhudumia shughuli za utafiti wa gesi na mafuta baharini. Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu iliyopendekezwa.

### v. Bandari ya Kigoma

Katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kuongeza kina cha eneo la kufikia meli bandarini. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa kuongeza kina cha eneo la kufikia meli bandarini Desemba, 2012 na ujenzi wa gati unaendelea. Aidha, upembuzi yakinifu wa mradi wa Bandari Kavu ya Katosho ulikamilika Juni, 2012 na tathmini ya fidia inaendelea kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kigoma mjini.

### vi. Bandari ya Mbegani Bagamoyo

Katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kufanya tathmini ya fidia kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Mbegani Bagamoyo. Kazi inayoendelea ni kumtafuta mzabuni wa kufanya tathmini ya fidia kwa ajili ya hekta 1,048 zinazohitajika kwa mradi huo. Aidha, Upembuzi yakinifu umekamilika na kubainisha kuwa Bandari ya Bagamoyo itakuwa ya kisasa yenye kina cha mita 14.

### vii. Bandari ya Kasanga

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2012/13, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutafuta mbia atakaeshirikiana na TPA kujenga gati mbili pamoja na uendeshaji wa bandari hiyo umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia mizigo ulikamilika.

## B. Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme

### a) Bomba la Gesi (Mtwara - Dar es Salaam)

Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 93.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa bomba la Gesi lenye urefu wa km 532 (Mtwara– Dar es Salaam) na kipenyo cha inchi 36 yameanza ambapo jiwe la msingi liliwekwa Novemba, 2012 na mabomba yameshaanza kusambazwa katika njia litakapopita bomba hilo. Aidha, fidia ya ardhi kupisha ujenzi imekamilika ambapo wanakijiji wapatao 3,092 wamelipwa. Jumla ya kiasi cha fedha kilichotumika katika fidia ni shilingi 6,857,746,020.

### b) Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi (MW 240)

Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 5 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Kinyerezi (Dar es salaam). Mradi huu unagharimiwa kwa mkopo kutoka *Japan Bank of International Corporation* ambao watachangia asilimia 85 na benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini itachangia asilimia 15 ya gharama za mradi. Ujenzi wa mradi huu utagharimu kiasi cha Dola za Kimarekani 432,137,936. Utekelezaji wa mradi huu haujaanza kutokana na kuchelewa kwa majadiliano ya mkopo kati ya Serikali na *Japan Bank of International Corporation* na kigezo cha kufanya uhakiki wa mradi kilichowekwa na benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini.

### c) Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi (MW 150)

Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 13 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na Serikali kuingia mkataba na Mkandarasi (Jacobsens), kumlipa mkandarasi kiasi cha shilingi bilioni 13 na mkandarasi kukabidhiwa eneo la kazi na kuanza maandalizi ya ujenzi.

### d) Makaa ya Mawe Kiwira (200 MW)

Kwa mwaka 2012/13, mradi umetengewa shilingi bilioni 40.0 zitakazotumika kulipia madeni ya mgodi na kufanya tafiti kwa ajili ya mtambo na njia ya umeme. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kulipwa kwa stahiki za wafanyakazi, sehemu ya madeni ya mradi kutoka Benki za CRDB, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF); na kuweka saini *Deal of settlement* na *Head of deal* kati ya Serikali na *Tanpower Resources* kuhusu mradi wa Kiwira. Mchakato wa ukamilishaji wa malipo kwa Kampuni ya *TanPower Resource* ili iweze kukabidhi mradi kwa Shirika la Madini la Taifa (State Mining Coorporation) unaendelea.

**e) Umeme wa Msongo wa 220 Kv (North – West Grid)**

Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 5 zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa gridi ya Kaskazini-Magharibi yenye msongo wa 220Kv kutoka mkoa wa Shinyanga (Bulyanhulu) hadi Mbeya kupitia mikoa ya Kigoma na Rukwa. Mchakato wa kutafuta fedha za kutosha za kuwezesha ujenzi wa mradi huu zinaendelea. Gharama za mradi ni dola za Kimarekani milioni 664.

**f) Umeme wa Msongo wa 400 Kv (Iringa-Shinyanga)**

Katika mwaka 2012/13, kiasi cha shilingi bilioni 5, fedha za ndani na shilingi bilioni 7.5, fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia kuu ya umeme wa Kv 400 yenye urefu wa km 670 kutoka Iringa kupitia Dodoma, Singida mpaka Shinyanga ili kuimarisha usafirishaji wa umeme kwenye njia ambayo sasa ina uwezo wa kusafirisha umeme wa Kv 220. Hatua iliyofikiwa ni malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi na kutangaza zabuni za wakandarasi wa ujenzi wa njia na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme.

**g) Umeme wa Msongo Kv 132 (Makambako - Songea)**

Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 2 fedha za ndani na shilingi bilioni 7.5 fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya Kv 132 ya urefu wa km 250 kutoka Makambako hadi Songea, vituo vya kupoza umeme wa Kv 132/33 vya Madaba na Songea. Kazi iliyofanyika mpaka sasa ni kupitia upya michoro (upgrading & design) kutoka msongo wa Kv 132 na kuwa Kv 220 ili kukidhi mahitaji ya umeme katika miradi ya Ngaka, Mchuchuma na Liganga. Aidha, wakandarasi wa mradi huu (usafirishaji – kilomita 250 na wasambazaji kilomita 900) wamepatikana. Uhakiki na uwekaji wa alama (demarcation along the line corridor) katika njia ya umeme wa msongo wa Kv 220 unaendelea. Fidia itafanyika baada ya kukamilika kwa zoezi la uwekaji wa alama eneo la mradi.

**h) Mradi wa Murongo-Kikagati**

Kwa mwaka 2012/13 shilingi bilioni 12.0 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ambao unatekelezwa kwa ushirikiano na Serikali ya Uganda. Utekelezaji wa mradi huu haujaanza kutokana na Serikali ya Tanzania na Uganda kuanza majadiliano upya kwa ajili ya kuboresha mkataba wa awali kwa maslahi ya pande zote mbili. Mradi huu utakapokamilika utawezesha kila nchi kupata MW 8.

## C. Barabara, Madaraja na Vivuko

### a) Barabara kuu

Katika mwaka 2012/13, mafanikio yaliyopatikana katika eneo la barabara ni pamoja na:-ujenzi wa kilomita 170.6 ikilinganishwa na lengo la kilomita 414 za barabara kuu kwa kiwango cha lami; na ukarabati wa kilomita 64.57 dhidi ya lengo la kilomita 135 za barabara kuu kwa kiwango cha lami.

### b) Barabara Zenye Kufungua Fursa Kiuchumi

Katika mwaka 2012/13, barabara zilizokusudiwa kujengwa na kukarabatiwa katika eneo hili zipo katika maeneo maalum kama vile Ukanda Maalum wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) ambapo barabara ya Kidatu-Ifakara-Lupilo-Malinyi-Londo-Lumecha/Songea pamoja na ujenzi wa Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi-Ifakara-Mahenge. Utekelezaji ni: mchakato wa kumpata Mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Kidatu-Ifakara-Lupilo-Malinyi-Londo-Lumecha/ Songea unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

### c) Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani

Barabara ya Arusha – Namanga, ukarabati umekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) na ulizinduliwa Novemba 2012; Tanga – Horohoro, ujenzi umekamilika chini ya ufadhili wa *Millenium Challenge Coorperation* (MCC); Barabara ya Nyanguge – Musoma, ukarabati unaendelea sehemu ya Mwanza/Mara Boarder – Musoma (km 85); na Barabara ya Usagara – Kisesa, mchakato wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi uko kwenye hatua za mwisho.

### d) Barabara za Mikoa

Katika mwaka 2012/13, ujenzi na ukarabati kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha barabara zinazounganisha mikoa hapa nchini utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Ujenzi wa Kilometa 8.2 ikilinganishwa na lengo la kilometa 31.9 kwa kiwango cha lami; ukarabati wa kilometa 99.45 ikilinganishwa na lengo la kilometa 573.6 za barabara za mikoa kwa kiwango cha changarawe.

### e) Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini

Katika eneo hili miradi iliyokusudiwa kutekelezwa ni: mradi wa kupunguza msongamano wa magari katika barabara za Jiji la Dar es Salaam. Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo: ujenzi wa barabara ya Kawawa –Msimbazi – Twiga

(Jangwani) umekamilika kwa asilimia 70; Ubungo – Terminal – Kigogo imekamilika kwa asilimia 100; Jet Corner – Vituka – Davis Corner, imekamilika kwa asilimia 90; Ubungo Maziwa – External imekamilika kwa asilimia 40. Barabara ambazo kazi ya usanifu imekamilika ni; Tabata dampo – Kigogo, Kimara – Kilungule - External, Mbezi – Malambamawili - Kinyerezi – Banana, Tegeta – Kibaoni – Wazo – Hill – Goba - Mbezi Luis, Tangi Bovu – Goba, Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni na Flyovers za Dar es Salaam.

**f) Madaraja na Vivuko**

Madaraja na vivuko ambavyo vilipangwa kujengwa katika mwaka 2012/13 ni pamoja na: daraja la Nanganga - kazi za ujenzi zimekamilika; daraja la Nangoo - kazi za ujenzi ziko kwenye hatua za mwisho; daraja la Malagarasi - kazi za ujenzi zinaendelea na ujenzi umekamilika kwa asilimia 85; daraja la Kilombero - Mkandarasi amepatikana na vifaa kwa ajili ya ujenzi vimeshafikishwa eneo la kazi; daraja la Kigamboni – uzinduzi ulifanyika Septemba, 2012 ambapo kazi ya ujenzi imeshaanza; na daraja la Kirumi – mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata Mtaalam Elekezi kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea. Aidha, ujenzi wa kivuko cha Rugenzi na maegesho ya magari kwenye kivuko cha Kisongo – Rugezi umekamilika Septemba, 2012.

**D. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**a) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

Katika kuhakikisha uwepo wa mawasiliano ya uhakika nchi nzima, kiasi cha shilingi bilioni 2.0 zilitengwa ili kutandaza nyaya na miundombinu ya vituo vya takwimu mwaka 2012/13. Hadi Desemba 2012, mikoa iliyosalia ilikuwa imeunganishwa katika mkongo wa Taifa. Vilevile, nchi jirani (isipokuwa Msumbiji) zimeunganishwa na Mkongo na zimeanza kuutumia. Kampuni kubwa zilizounganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi sasa ni Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), TIGO, Zantel, Vodacom, Airtel, pamoja na Simba Net. Aidha, kampuni za nje ya nchi zilizounganishwa na mkongo ni UCOM na ECONET (Burundi), MTN na Airtel (Zambia), MTL (Malawi) na RDB, MTN,Airtel na KDN (Rwanda).

**b) Maendeleo ya TEHAMA**

Mwaka 2012/13, shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa kuimarisha vituo vya mawasiliano vijijini ili kuwezesha kupanua mtandao wa mawasiliano nchi nzima. Hatua iliyofikiwa ni kukamilisha taarifa na tathmini ya vituo 15 (Mrijochini, Ikungi, Hai, Wete, Kilolo, Masota-A Tegeta, Bagamoyo, Karagwe, Isaka, Mbozi, Namtumbo, Rorya, Masasi,

Ludewa na Mpanda, vilivyojengwa miaka ya nyuma ili vituo hivyo viweze kuboreshwa.

**c) Maeneo Maalum ya TEHAMA *(ICT Park)*, Dar es Salaam**
Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 5.0 zimetengwa kwa ajili ya taratibu za kulipa fidia ya ardhi katika eneo la Kigamboni na kuanza kuweka miundombinu muhimu kwa ajili ya kituo cha mawasiliano. Kumekuwa na changamoto katika eneo lililoainishwa awali, hivyo Tume ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaendelea na mazungumzo ya kupata eneo jingine la *ICT Park* na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Kigamboni) na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo na EPZ (Bagamoyo). Hata hivyo, Mpango kazi unaobainisha shughuli zitakazotekelezwa katika *ICT Park* umeshaandaliwa, mafunzo kwa watakaoshiriki katika *ICT Park* yanaendelea na utaratibu wa kutafuta wabia zaidi unaendelea. Wabia walioonyesha nia ya uwekezaji mpaka sasa ni Seacom International na Smart Village.

**d) Anuani za Makazi na Simbo za Posta**
Katika mwaka 2012/13, shilingi milioni 709.5 zilitengwa kutekeleza mfumo wa uwekaji anuani kwa kutumia majina ya mitaa na majengo ili kuhakikisha maeneo ya watu binafsi na biashara yanatambuliwa. Uzinduzi wa mradi wa anuani za makazi na simbo za posta ulifanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam Septemba, 2012. Utekelezaji wa mradi ulianza katika mkoa wa Dar es salaam kwa manispaa zote kuanza kuipa mitaa majina. Hadi sasa, Manispaa ya Kinondoni imekamilisha utoaji wa majina katika mitaa kwa maeneo yaliyopimwa, tayari kwa kuweka vibao vya majina ya mitaa na namba za nyumba. Aidha, manispaa za Temeke na Ilala zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha zoezi hilo.

## E. Maji safi na Majitaka

**a) Kuboresha huduma za maji katika jiji la Dar es Salaam**
Mwaka 2012/13, shilingi bilioni 118.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 68.8 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi wa maji la Ruvu Chini na Ruvu Juu na mtandao wa usambazaji maji. Utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatavyo:

**b) Mradi wa Maji Ruvu Chini**
Upanuzi wa mradi wa Maji wa Ruvu Chini unaendelea ambapo utaongeza uwezo wa sasa wa mita za ujazo 182,000 kwa siku hadi 270,000 kwa siku ili kukidhi mahitaji ya maji hadi mwaka 2032. Mkataba wa miezi 15 wa ujenzi

wa bomba la Ruvu Chini ulisainiwa Septemba 2012 kati ya DAWASA na SINO HDYRO kutoka China. Kiasi cha shilingi bilioni 18.3 zimetolewa ikiwa ni malipo ya awali kwa ajili ya kumlipa mkandarasi. Mkataba wa kusimamia ujenzi ulisaniwa kati ya Dar es Salaam Water Sewage Authority (DAWASA) na MS Gauff Ingeniere toka Ujerumani. Tathmini ya fidia ya shilingi milioni 900 iliyofanyika mwaka 2010, imeshalipwa yote hadi kufikia Januari, 2013 ili kupisha ujenzi wa bomba kuu la Ruvu Chini. Aidha, upimaji na uchunguzi wa njia ya bomba unaendelea.

**c) Mradi wa Maji Ruvu Juu**

Usanifu wa upanuzi wa mtambo umekamilika ambapo ilipendekezwa kupanua mtambo kutoka uwezo wa sasa wa mita za ujazo 82,000 kwa siku hadi mita za ujazo 196,000 kwa siku ili kukidhi mahitaji ya maji hadi mwaka 2032. Kutokana na mabadiliko ya kuongeza uzalishaji, bomba lenye kipenyo cha mm 900 la urefu wa km 20 lililopendekezwa awali litabadilika, sasa yatalazwa mabomba matatu, yaani bomba jipya lenye kipenyo cha mm 1200 na urefu wa km 41 kutoka Mlandizi hadi Kibamba, na bomba la 900 mm na urefu wa km 21 kutoka Kibaha (TANITA) hadi Kibamba na bomba la 1000 mm, 10km kutoka Kibamba hadi Kimara pamoja na ujenzi wa tangi lenye ujazo wa 40,000 $m^3$ eneo la Kibamba. Mtaalam Mshauri amekamilisha usanifu wa mabomba na njia za mabomba. Ujenzi wa mradi huu utagharamiwa na fedha kutoka Serikali ya India na tayari zabuni ya ujenzi imeshatangazwa.

**d) Ujenzi wa Bwawa la Maji Kidunda**

Ripoti ya mwisho ya Mazingira (Environment and Social Management Plan - ESMP) imepokelewa Agosti 2012 na kuwasilishwa Baraza la Taifa la Mazingira mwezi huo ili kupata kibali cha mazingira. Hati ya Makubaliano kati ya DAWASA na TANESCO kuhusiana na umeme utakaozalishwa Kidunda imekamilika. Uthamini wa fidia kwa eneo linalozunguka bwawa ulifanyika mwaka 2012, na thamani yake ni shilingi bilioni 3.2 ambapo bado wananchi hawajalipwa. Tathmini ya fidia kwa kaya 500 zilizo kandokando ya barabara ya Kidunda kupisha upanuzi wa barabara ya Kidunda-Ngerengere imeanza na itakamilika Aprili 2013. Serikali ya China imeonyesha nia ya kufadhili ujenzi wa bwawa kwa kutoa mkopo wenye masharti nafuu.

**e) Mradi wa Visima Virefu Kimbiji na Mpera**

Mradi huu unahitaji ulipaji wa fidia kwenye maeneo ya kuzunguka visima, eneo lote la mradi, na eneo la kujenga matanki ya kuhifadhi maji. Tathmini ya fidia eneo la mita sitini kuzunguka kila kisima ilifanyika mwaka 2009 kwa

Kimbiji na 2010 kwa Mpera ambapo thamani yake ni jumla ya shilingi milioni 638,288. Fidia hii tayari imeshalipwa kwa wananchi 67 wa Kimbiji na 63 wa Mpera. Tathmini katika maeneo yatakapojengwa matanki ya kuhifadhia maji (Luzando na Kisarawe II) umekamilika Desemba 2012 na thamani ya fidia kwa Luzando ni shilingi milioni 287 na Kisarawe II ni Shilingi bilioni 1.3. Fedha hizo bado hazijalipwa. Aidha, tathmini ya eneo lote la Kimbiji iko katika hatua ya uhakiki, na kwa upande wa Mpera bado haijaanza. Pamoja na changamoto hizo, utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo mshauri mwelekezi anaendelea na mapitio ya usanifu wa mabomba makuu na matenki ya kuhifadhi maji yatakayozalishwa Kimbiji na Mpera na usanifu umeshakamilika. Ufuatiliaji wa vibali vya kupitisha mabomba katika maeneo ya: Jeshi, SONGAS, bomba la mafuta la Tanzania na Zambia (TAZAMA), reli ya TAZARA na Wakala wa Barabara Nchini (Tanzania National Road Agency) unaendelea. Vile vile, majadiliano na Shirika la Umeme Tanzania (*Tanzania National Electricity Supply Company*) kuhusu upatikanaji wa umeme katika maeneo ya mradi yanaendelea.

**f) Mradi wa Maji Mbeya**

Katika mwaka 2012/13 Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji katika jiji la Mbeya. Mradi huu ulihusisha ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kitekeo cha maji eneo la Imeta, Iyela, Ivumwe na Halewa; Ujenzi wa matanki eneo la Forest, Iwambi, Iganzo, VETA, Iganjo, Nsoho, na Idunda yenye ujazo wa mita 6,900 za kuhifadhia maji. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ulihusisha ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 56.8 na mabomba ya usambazaji maji kilomita 280.15. Mradi huu umezinduliwa rasmi Julai 2012 na unauwezo wa kuhudumia wakazi wapatao 490,000.

**g) Miradi ya Maji Vijijini**

Serikali imeendelea kuboresha huduma za maji vijijini kwa kujenga miradi mipya, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji katika halmashauri. Uboreshaji huo unatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kusanifu, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Idadi ya wananchi wanaoishi vijijini ambao wanapata huduma ya maji safi, salama, na ya kutosha karibu na makazi umeongezeka kutoka watu 16,308,651 ambao ni sawa na asilimia 53.74 ya watu wote waishio vijijini mwezi Desemba mwaka 2005 hadi kufikia watu 20,634,227 ambao ni sawa na asilimia 56.57 ya watu wote waishio vijijini mwezi Desemba mwaka 2012.

### 2.3.2 Kilimo

**a) Kilimo cha Miwa**

Katika kuendeleza kilimo cha miwa kwa mwaka 2012/13, mashamba kwa ajili ya uwekezaji katika mabonde ya Wami, Ruvu, Kagera, Kilombero na Malagarasi kiasi cha hekta 277,000 yametambuliwa na uhakiki unaendelea ili kupisha uwekezaji. Aidha, maandalizi ya mpango wa matumizi wa eneo hilo yanaendelea.

Wawekezaji walioonesha nia ni:- Kampuni ya Ecoenergy (bonde la Ruvu - hekta 20,373.56); Frontline Development Partners (Mkongo, Rufiji - hekta 20,000); Agroforestry (Muhoro Rufiji- hekta 20,000); na Rufiji Sugar (Tawi/ Utuge - hekta 20,000). Wawekezaji hawa wanatarajia kushirikiana na wakulima wadogo. Shamba la ukubwa wa hekta 50,000 katika eneo la Mkulazi (Morogoro) limepatikana na utafiti wa maji unaendelea.

**b) Miradi ya Ukanda wa SAGCOT**

*i. **Mradi wa Mpanga –Ngali mila, Morogoro** (Hekta 31,500)*

Katika mwaka 2012/13 shilingi bilioni 1.0 zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa michoro ya skimu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo. Utekelezaji ni: maandalizi ya upembuzi yakinifu yamekamilika, ambapo taarifa kuhusiana na uwanda (topography), hali ya udongo, rasilimali ya maji, hali ya mazingira na uchambuzi wa faida na hasara za mradi zitakusanywa na kutathminiwa kwa lengo la kuandaa zabuni ya kuendeleza skimu.

*ii. **Mradi wa Umwagiliaji – Itete, Morogoro** (Hekta 1000)*

Katika mwaka 2012/13 shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji. Utekelezaji ni: uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa skimu yenye uwezo wa kumwagilia hekta 1,000 umekamilika.

*iii. **Mradi wa Umwagiliaji Sonjo, Morogoro** (Hekta 300)*

Katika mwaka 2012/13, shilingi milioni 600 zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo na kuwawezesha kuzalisha kwa tija zaidi na kuingia katika kilimo cha kibiashara cha miwa. Utekelezaji ni: upembuzi yakinifu umeanza ambapo taarifa kuhusiana na uwanda (topography), hali ya udongo, rasilimali ya maji, hali ya mazingira na uchambuzi wa faida na hasara za mradi zimekusanywa na ukokotoaji na tathmini uko katika hatua mbalimbali. Uandishi wa taarifa umefikia asilimia 65, ukusanyaji takwimu kuhusiana na uwanda (topography), hali ya udongo na rasilimali ya maji umefikia asilimia 60, 90 na 50 kwa mtiririko huo.

*iv. Mradi wa Umwagiliaji Lupilo, Morogoro (Hekta 4,000)*
Katika mwaka 2012/13 shilingi bilioni 1.0 zimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa michoro ya skimu ya umwagiliaji. Utekelezaji ni: maandalizi ya upembuzi yakinifu yamekamilika ambapo taarifa kuhusiana na uwanda (topography), hali ya udongo, rasilimali ya maji, hali ya mazingira na uchambuzi wa faida na hasara za mradi zitakusanywa na kutathminiwa kwa lengo la kuandaa zabuni ya kuendeleza skimu.

**c) Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Chakula**
Katika mwaka 2012/13, shilingi bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maghala manne ya kuhifadhia chakula (transit shed) katika maeneo ya Sumbawanga, Mpanda, Mbozi na Songea. Utekelezaji ni: kuanza maandalizi ya ujenzi wa ghala la kuhifadhia nafaka katika kanda ya Songea, lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000. Michoro kwa ajili ya ghala na taratibu za zabuni kwa ajili ya kupata mkandarasi wa ujenzi zimekamilika ambapo ujenzi utaanza Aprili 2013 na unatarajiwa kukamilika Juni 2013. Uzoefu utakaopatikana katika ujenzi wa ghala Songea utatumika katika ujenzi wa maghala ya Sumbawanga, Mpanda na Mbozi katika mwaka 2013/14.

Mafanikio Mengine katika Sekta ya Kilimo ni kama ifuatavyo:

i. Mashamba ya mfano kwa ajili ya kilimo cha mpunga yaliandaliwa katika skimu za umwagiliaji za Mgololo (Mufindi) – hekta 700; Ngana (Kyela) – hekta 200; Makwale (Kyela) – hekta 70; Kidogozelo (Bagamoyo) – hekta 25; Ilonga (Kilosa) - hekta 120, Mvumi (Kilosa) - hekta 720; Rudewa (Kilosa) – hekta 500; Kinyope (Lindi) – hekta 600; na Kitere (Mtwara) – hekta 200;
ii. Ununuzi wa tani za ujazo 32,801.606 za mahindi na tani 2,308 za mtama sawa na asilimia 16.4 ya lengo kwa mwaka;
iii. Mpango wa vocha kwa mwaka 2012/13 ulikamilika, na takriban vocha 421,375 za mbegu bora na mbolea zilisambazwa katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Morogoro, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Geita, Kagera, na Mara;
iv. Maduka 180 ya wasambazaji wa viuwadudu yalikaguliwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, ambapo kati ya hayo maduka 70 yalifungwa kutokana na kutozingatia sheria;
v. Operesheni ya kudhibiti nzige ilifanyika katika maeneo ya Iku-Katagi, Malagarasi na Wembere ambapo jumla ya hekta5,700 zilizokuwa na nzige zilinyunyiziwa dawa lita 2500; na
vi. Teknolojia za kilimo zilisambazwa kwa wadau wakati wa maonesho

ya nane nane, ikiwa ni pamoja na teknolojia ya matumizi ya uyoga, uzalishaji bora wa mbogamboga, na utoaji wa mafunzo juu ya masoko, kuongeza thamani ya mazao na umwagiliaji wa matone.

### 2.3.3 Viwanda

**a) Mradi wa Mchuchuma na Liganga**

Katika mwaka 2012/13, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya kuimarisha barabara za Itoni – Mkiu – Mchuchuma na Mkiu – Liganga; na kuongeza ujuzi kwa wataalam wa ndani kwa ajili ya utekelezaji mradi. Utekelezaji ni: kuanza upembuzi yakinifu na kukarabati sehemu korofi za barabara.

**b) Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Pwani**

Katika mwaka wa fedha 2012/13, kiasi cha shilingi bilioni 3.26 kimetengwa kwa ajili ya: malipo ya mhandisi mshauri; kutoa mafunzo kwa wataalam wa kuendesha kiwanda (skills transfer); ujenzi wa mfumo wa maji safi na majitaka; na usanifu wa kituo cha umeme kwa eneo la TAMCO. Hatua za utekelezaji ni: ujenzi wa majengo ya kiwanda umekamilika; na usanifu wa kina wa kiwanda na mitambo umekamilika. Aidha, juhudi za kuleta miundombinu muhimu, ikiwa ni pamoja na umeme, maji safi na majitaka na barabara zinaendelea ambapo bomba lenye kipenyo cha milimita 75 la maji ya kiwanda limeunganishwa. Uunganishwaji wa umeme utakamilika baada ya kufunga transfoma za kiwanda.

**c) Eneo la Viwanda la TAMCO**

Eneo la viwanda la TAMCO - Kibaha linakusudiwa kuwa na viwanda vidogo na vya kati. Michoro ya eneo la wazi lenye ukubwa wa hekari 88 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika eneo la mradi umekamilika. Zoezi la upimaji wa viwanja na maeneo ya miundombinu limekamilika na kuidhinishwa. Usanifu wa kina wa miundombinu ya barabara, maji safi na maji taka umekamilika. Kazi inayofuata ni ujenzi wa miundombinu hususan barabara kwa ajili ya wawekezaji.

**d) Mradi wa Magadi soda - Bonde la Engaruka**

Katika mwaka 2012/13, Serikali imetenga shilingi milioni 700 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kuchimba visima 12. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni: uchorongaji wa mashimo 12 kwa ajili ya kuhakiki wingi na ubora wa magadi umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kukusanya taarifa za uwekezaji kwenye mradi huo.

**e) Maeneo Maalum ya Uwekezaji**

Mwaka wa fedha 2012/13, kiasi cha shilingi bilioni 50.2 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ulipaji fidia katika maeneo maalum ya uwekezaji - *Export Processing Zones* (EPZ) Bagamoyo na Kigoma. Tathmini ya fidia katika eneo la Bagamoyo ilifanyika 2011 na thamani yake ni shilingi billioni 58.8 na katika eneo la Kigoma tathmini ilifanyika 2010 kwa thamani ya shilingi 2.8 bilioni. Utekelezaji ni: jumla ya shilingi bilioni 16.9 zimelipwa kama fidia kwa awamu ya kwanza (Julai 2012) na ya pili (Januari 2013) katika eneo la Bagamoyo ambapo jumla ya eneo lililokwishalipiwa fidia ni hekta 1,600 kati ya hekta 5,700. Kwa upande wa Kigoma kwa mwaka huu hakuna malipo yaliyofanyika hadi sasa, hata hivyo malipo ya shilingi 1.5 billioni yalishafanyika mwaka 2011/12 kwa hekta 3,000 kati ya hekta 20,000. Aidha Mpango Kamambe wa eneo maalum la uwekezaji Bagamoyo umekamilika.

### 2.3.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu

Katika kutumia fursa za rasilimali zilizopo nchini, Serikali imeazimia kuendeleza ujuzi katika nyanja maalum hasa utaalamu na ujuzi katika gesi na mafuta, chuma, urani na madini mengine. Kiasi kilichotengwa kutoka kwenye utafiti na maendeleo ni shilingi bilioni 21.5 fedha za ndani na shilingi milioni 975.9 fedha za nje. Hadi kufikia nusu mwaka, wataalamu wapatao 295 wameendelea kugharimiwa. Kati ya hao, 195 ni wa shahada ya uzamili na 100 ni wa uzamivu na wanasoma katika vyuo vikuu 5 vya umma ambavyo ni Dar-es Salaam, Sokoine, Muhimbili, Ardhi na Nelson Mandela. Aidha, miundombinu imeendelea kuboreshwa katika vyuo vikuu, vyuo vya ustawi wa jamii na taasisi mbalimbali za utafiti.

### 2.3.5 Huduma za Utalii na Fedha

**a) Utalii**

Katika mwaka 2012/13, fedha zimetengwa kwa Chuo cha utalii Dar es Salaam iii kuboresha mazingira ya chuo na kutoa elimu bora. Hatua za utekelezaji zilizofikiwa ni pamoja na: kuendelea kuboresha mazingira ya utoaji taaluma.

**b) Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

Katika mwaka 2012/13 Serikali ililenga kuharakisha uanzishwaji na kuongeza mtaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Hatua zifuatazo zimefikiwa ni: usajili ulifanyika Septemba, 2012 na kupewa namba 94075; mchakato wa kuunda bodi ya wakurugenzi na kuajiri maafisa waandamizi

unaendelea; jengo la ofisi limepatikana Dar es Salaam (Jengo la Shirika la Nyumba - mtaa wa Samora) na kiasi cha sh. bilioni 60 kimeshatolewa kama kianzio cha mtaji.

**c) Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB)**

Katika kuongeza mtaji katika Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) ili kuweza kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya maendeleo nchini, jumla ya shilingi bilioni 50 zimeongezwa kama mtaji, na hivyo kuifanya benki hiyo kuwa na mtaji wa shilingi bilioni142.14. Kwa vigezo vya Benki Kuu, benki za maendeleo zinahitaji kuwa na kiwango cha chini cha mtaji wa shilingi bilioni 50 ili ziweze kujiendesha kibiashara na kufungua matawi. Katika mwaka 2012/13, tawi la TIB Mbeya lilianza rasmi kutoa huduma na hivyo kuwa na jumla ya matawi matano ambayo ni Mbeya, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam (Samora na Mlimani).

**d) Benki ya Wanawake Tanzania**

Katika kuiongezea mtaji Benki ya Wanawake Tanzania, ili iweze kuhimili ushindani katika soko na kuwa benki ya kibiashara, Benki ilipewa jumla ya shilingi milioni 200 na hivyo kuifanya benki hiyo kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 7. Aidha, kutokana na vigezo vya Benki Kuu ya Tanzania, benki hii inahitaji kuwa na mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 15 ili kujiendesha kibiashara na kufungua matawi. Aidha, kutokana na mtaji kuwa mdogo, inakuwa vigumu kuingia katika soko la hisa.

### 2.3.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Utekelezaji wa shughuli za kikanda na kimataifa katika nusu mwaka 2012/13 ni kama ifuatavyo: ujenzi wa Makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikamilika na kuzinduliwa mwezi Novemba, 2012; ujenzi wa vituo vya utoaji huduma kwa pamoja mipakani (One Stop Border Post) uliendelea katika mipaka baina ya Tanzania na nchi wanachama wa Afrika Mashariki katika maeneo ya Sirari/ Isebania (70%), Horohoro/Lungalunga (80%), Mtukula/Mtukula, Namanga/Namanga (10%) na Holili/Taveta (80%). Vituo hivi vitapunguza muda wa kukamilisha taratibu za uvukaji mipakani hivyo kurahisisha usafiri na usafirishaji; na kukamilika kwa Mkakati wa Taifa wa utekelezaji wa itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 2.4 Maeneo Mengine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi

### 2.4.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Katika mwaka 2012/13, miradi iliyokusudiwa kutekelezwa katika eneo la

elimu na mafunzo ya ufundi imejumuisha: uendelezaji wa ujenzi wa vyumba vya mihadhara, maktaba, mabweni ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya ufundi; kusaidia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES I); ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya ualimu; na ujenzi na ukarabati wa Maktaba. Utekelezaji ni kama ifuatavyo:

a) **Chuo Kikuu cha Udaktari Mloganzila, Dar es Salaam**
Serikali ya Korea ya Kusini imekubali kutoa mkopo wa masharti nafuu kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 76.5 sawa na shilingi bilioni 121 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali na kuweka vifaa tiba. Serikali itachangia shilingi 7,281,196,000 ili kukamilisha miundombinu ya barabara, maji na umeme na shilingi 603,093,396,136 kwa ajili ya majengo na miundombinu mengine ya chuo. Utekelezaji ni: Upelekaji wa umeme katika eneo la ujenzi uko katika hatua za mwisho ambapo Transfoma imeshanunuliwa; mchakato wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami na upelekaji wa maji kutoka Kibamba CCM hadi eneo la ujenzi unaendelea.

b) **Chuo Kikuu Dodoma na Mzumbe**
Ujenzi wa maabara ya Chuo cha Sayansi za Asili na Hisabati unaendelea katika chuo kikuu cha Dodoma. Ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wasichana kampasi ya Morogoro na ukumbi wa mihadhara na maktaba katika kampasi ya Mbeya ya Chuo Kikuu Mzumbe unaendelea.

c) **Chuo cha Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela**
Kwa mwaka 2012 chuo kimeweza kukarabati na kuboresha majengo yaliyorithiwa kutoka CAMARTEC, kujenga mabweni mawili kwa ajili ya wanafunzi wa shahada ya uzamili, kuzungushia uzio na kukarabati barabara za ndani ya chuo kwa kiwango cha changarawe pamoja na kuchimba visima viwili virefu vyenye uwezo wa kutoa maji kiasi cha mita za ujazo 46 kwa saa. Katika kuboresha elimu inayotolewa chuoni hapo, chuo kinaendelea na utaratibu wa kuweka maabara na kuongeza vyumba vya madarasa na ofisi. Aidha katika mwaka 2012 chuo kimedahili wanafunzi 39 wa ngazi ya Uzamili na 54 wa Uzamivu katika fani tano zinazotolewa chuoni hapo.

d) **Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu**
Ujenzi wa vyuo na uwekaji wa umeme katika Chuo cha Ualimu Ndala Tabora umekamilika. Aidha, ukarabati wa bweni na choo cha wavulana katika chuo cha Ualimu Kitangali, Mtwara na vyoo vya wasichana katika Chuo Ualimu Butimba, Mwanza umekamilika na vyumba vya madarasa vilivyoezuliwa na kimbunga katika chuo cha Ualimu Tarime vimekarabatiwa.

e) **Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi na Maendeleo ya Jamii**
Ukarabati wa majengo na miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Same na Misungwi umekamilika, na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya kimewekewa umeme wa jua. Aidha, kwa upande wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi – VETA, mafunzo ya wakufunzi yamefanyika na wanafunzi 813 wamedahiliwa kati ya 1250 wanaotakiwa. Vilevile, ujenzi wa karakana 5 na ukarabati wa vyuo viwili vya Mputa na Mhukuru unaendelea.

Mafanikio mengine katika elimu na mafunzo ya ufundi ni pamoja:

i) Kuboreshwa kwa uwiano wa kitaifa wa mwalimu kwa wanafunzi kutoka 48 mwaka 2011 hadi 46 mwaka 2012 kwa shule za msingi;
ii) Kuboreshwa kwa uwiano wa walimu wenye sifa katika shule za msingi na sekondari kutoka 49 na 34 mwaka 2011 hadi 47 na 29 mwaka 2012;
iii) Kuboreshwa kwa uwiano wa walimu wa vyuo vya ualimu kutoka 23 mwaka 2011 hadi 22 mwaka 2012; na
iv) Walimu 1,056 wa ngazi ya stashahada, 25,626 walimu wa cheti daraja A na walimu 51 wa elimu maalum wamehitimu.

### 2.4.2 Afya na Ustawi wa Jamii

Katika sekta ya afya na ustawi wa jamii, programu na miradi iliyokusudiwa kutekelezwa mwaka 2012/13 ni pamoja na:- (i) Mpango wa Usimamizi wa Sekta ya Afya; (ii) Kuwezesha Programu ya kupunguza vifo vya kinamama wajawazito; ( iii) Kuimarisha huduma za tiba kwa kuimarisha hospitali za Rufaa; (iv) Kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya magonjwa ya Saratani Ocean Road, Kituo cha Tiba ya Magonjwa ya Koo kilichopo Hospitali ya Muhimbili na kujenga na kukarabati majengo ya hospitali ya mkoa wa Mtwara, Mara na Lindi. Utekelezaji ni:

i. Hospitali ya Saratani Ocean Road: uwekaji wa samani za ofisini, vifaa vya kliniki na vitanda vya wagonjwa umekamilika kwa asilimia 98. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na shirika la *International Atomic Energy Agency* (IAEA) wanategemea kufunga *Gama* kamera. Aidha, baadhi ya huduma za tiba zimeanza kutolewa ndani ya jengo hili;
ii. Hospitali ya Taifa Muhimbili: ujenzi wa maabara (Indoscopic laboratory) umekamilika kwa asilimia 98. Vifaa vya kisasa kama vile vitanda vya kawaida vya hospitali, vitanda maalum kwa ajili ya wagonjwa waliokwishapasuliwa moyo, Ventilater 10 na mashine ya

cath-lab imefungwa. Ujenzi wa "medicals gas" upo katika hatua za mwisho. Aidha, ujenzi wa wodi katika kituo cha tiba cha magonjwa ya koo unaendelea;

iii. Ujenzi wa uzio wenye urefu wa kilomita 2.7 katika Hospitali ya Rufaa Mtwara unaendelea; na

iv. Ujenzi na ukarabati wa majengo ya hospitali ya mkoa wa Mtwara na Lindi unaendelea. Vyumba vya Upasuaji vitano katika hospital za Mtwara na Lindi vimekamilika. Aidha, ujenzi na ukarabati wa jengo la kliniki ya Mama na Mtoto-MCH na Vituo vya afya umekamilika kwa asilimia 80.

### 2.4.3 Mifugo na Uvuvi

Katika sekta ya Mifugo na Uvuvi, programu na miradi iliyopewa kipaumbele kwa mwaka 2012/13 ni pamoja na: Kuendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *Agricultural Sector Development Programme* (ASDP) katika maendeleo ya sekta ndogo ya mifugo; kuimarisha uwezo wa kitaasisi na mifumo ya utoaji wa taarifa kwa ajili ya usimamizi majanga katika maendeleo ya sekta ya mifugo na uvuvi; kuwezesha mfumo wa utambuaji na ufuatiliaji wa mifugo Tanzania; na kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Viumbe wa Bahari katika Ukanda wa Pwani. Utekelezaji ni:-

a. Vituo vya utafiti wa mifugo vimeendelea kuimarishwa kama ifuatavyo:-

i. Ukarabati wa maabara ya Embryo Transfer kituoni Mpwapwa Dodoma umekamilika kwa asilimia 80% ambapo kazi za kupaka rangi, kuweka vigae vya sakafu (tiles), kuweka milango na madirisha imekamilika. Pia, ukarabati wa ofisi kuu Mpwapwa umekamilika; na

ii. Ujenzi wa jengo la ofisi za Naliendele Mtwara uliendelea ambapo jengo la ofisi mpya liliezekwa na kuwekewa mfumo wa umeme.

b. Magonjwa ya Mifugo yameendela kudhibitiwa kama ifuatavyo:-

i. Jumla ya dozi 400,000 za dawa ya chanjo kwa ajili ya kukinga Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley Fever – RVF) zimenunuliwa kwa ajili ya Halmashauri za Manispaa na za Wilaya ili kukabiliana na ugonjwa huo pindi dalili za awali za ugonjwa huo zinapotokea. Halmashauri zilizopewa kipaumbele ni pamoja na Mkinga, Korogwe, Handeni, Kilindi, Simanjiro, Babati, Karatu, Ngorongoro, Monduli, Longido, Same, Rombo na Mwanga;

ii. Wizara kwa kushirikiana na GALVmed imeendelea kuhamasisha matumizi ya chanjo ya Ndigana kali ambapo ng'ombe 29,000

wamechanjwa dhidi ya Ndigana kali katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Morogoro. Mradi wa chanjo wa GALVmed umetoa dozi 55,000 zitakazotumika katika kipindi cha miezi 18 kwa mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya;

iii. Uchanjaji wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo umeendelea katika mikoa ya Manyara, Rukwa, Singida na Tanga kwa kutumia dozi 350,000 zilizotolewa na Shirika la Chakula Duniani (Food and Agricultural Organization) kwa Wizara;

iv. Jumla ya vyambo 9,286 vyenye viuatilifu aina ya pareto (Glossinex) vilitegwa katika wilaya za Urambo, Uvinza, Bagamoyo, Handeni, Pangani, Kaliua, Kisarawe, Kondoa, Mpanda , Nkasi, Nanyumbu, Kilombero, Mbulu na Manyoni. Aidha, mitego 12 (Biconical 6 na NGUU 6) ilitolewa kwa kila wilaya kwa uchunguzi wa mbung'o na bomba za mkono 14 "Hand Knapsack" zilitolewa, moja kwa kila wilaya ili kupulizia viuatilifu kwenye vyambo;

v. Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania imezalisha na kusambaza dozi 3,219,800 za chanjo ya mdondo, dozi 34,000 za Kimeta na dozi 26,500 za Chambavu;

vi. Wilaya 13 za Longido, Monduli, Hanang, Ngorongoro, Simanjiro, Mwanga, Meatu, Same, Kiteto, Kishapu, Arumeru, Maswa na Bariadi zimebainishwa ili kujengewa mitambo ya mfano inayozingatia hali ya ukame katika mazingira ya ufugaji wa asili. Aidha, mwongozo wa ujenzi, matumizi na uendeshaji wa mitambo hiyo unaandaliwa; na

vii. Ujenzi wa mfumo wa kuhifadhi taarifa za Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo umeanza ambapo taratibu za kupata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kujenga database hiyo zimefanyika.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Katika zoezi la utambuzi na usajili wa mifugo, taarifa muhimu zitakazoingizwa kwenye *database* zimekusanywa na zinachambuliwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ambapo wafugaji 2,428 walisajiliwa na ng'ombe 50,534 walitambuliwa kwa njia ya chapa ya moto katika vijiji 11;

ii. Vifaa 10,000 vya utambuzi wa mifugo vimenunuliwa (*Rumen Boluses* 5,000 na *management ear tags* 5,000);

iii. Kuwezesha uendeshaji wa Mamlaka ya Kusimamia shughuli za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Kusimamia uvuvi Bahari Kuu umekamilika;

iv. Kukamilisha marekebisho madogo katika jengo la Mvuvi (Kuweka

vigae kwenye eneo la juu ya jengo, pamoja na kukamilisha uunganishaji wa mfumo wa maji machafu kwenye mfumo wa Jiji);

v. Ujenzi wa ghala la kutunzia mazao ya mwani katika kijiji cha Jibondo, wilayani Mafia unaendelea. Aidha, maboya kwa ajili ya kuweka mipaka ya maeneo ya Hifadhi za Bahari yamenunuliwa; na

vi. Shirikisho la Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo (Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania) linaendelea na utaratibu wa kuanzisha Benki ya Wananchi wa mwambao wa Pwani (Coastal Community Banks) katika wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji. Mtalaam Mshauri anaendelea kuhamasisha wananchi kununua hisa ili kupata mtaji wakutosha kuanzisha benki.

### 2.4.4 Madini

Katika eneo hili, miradi itakayotekelezwa mwaka 2012/13 ni: Uendelezaji wa ujenzi wa ofisi za madini za mikoa: Mpanda, Mtwara, Dodoma, Geita na Arusha; utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (Sustainable Management of Mineral Resources Projects); kuendelea na ujenzi wa mtaro iii kuepusha mafuriko katika eneo lenye shimo la De Souza katika eneo la machimbo ya Mererani; na kuimarisha taasisi zinazoshughulika na tafiti za utafutaji na usimamizi wa madini. Utekelezaji ni: ukarabati wa ofisi za madini Geita na Arusha umekamilika; ujenzi wa mtaro wa De Souza katika maeneo ya Mererani kuepusha mafuriko umekamilika; zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa ofisi za madini za mikoa ya Katavi, Mtwara na Dodoma zimekamilika; mikataba kwa ajili ya utekelezaji wa *High resolution Airborne Survey* katka mikoa ya Morogoro, Mbeya, Katavi na Rukwa imekamilika na kuanza kutekelezwa; na mikataba ya usambazaji wa vifaa vya ugani kwa Geological Survey of Tanzania (GST), na vifaa na viambatishi (accessories) vya Tanzania Gemological Centre ilisainiwa.

### 2.4.5 Usafiri wa Anga

Mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha nusu mwaka 2012/13 kwa upande wa ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege ni kama ifuatavyo:-

i. Kukamilika kwa ujenzi wa tabaka la mwisho la lami kwa njia ya kutua na kurukia ndege (runway), njia ya kiungio (taxiway) na kuendelea kukamilisha tabaka la mwisho la lami kwa maegesho ya ndege (apron) katika kiwanja cha Songwe;

ii. Kukamilika kwa ujenzi wa tabaka la lami kwenye barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na maegesho ya magari na barabara za ndani kiwanjani, uchimbaji wa visima virefu vya maji, ujenzi wa msingi na nguzo za kubeba ghorofa ya kwanza kwa jengo jipya la

abiria na kuanza kutumika katika kiwanja cha ndege cha Songwe;

iii. Kuendelea kwa ujenzi wa tabaka la pili la lami (bitumen bound base) kwa barabara ya kuruka na kutua ndege kufikia mita 1,400 katika kiwanja cha ndege cha Kigoma;

iv. Kuendelea na hatua ya ujenzi wa tabaka la pili la barabara ya kuruka na kutua ndege kufikia mita 1400 katika kiwanja cha ndege cha Tabora;

v. Mkandarsi amesha kabidhiwa kazi na maandilizi ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza inaendelea;

vi. Kuendelea kwa ujenzi wa sehemu ya njia ya kurukia na kutua ndege, maegesho ya ndege na jengo la ablria katika kiwanja cha ndege Bukoba;

vii. Kukamilika kwa ujenzi wa maegesho, barabara ya kurukia na kutua ndege katika kiwango cha lami katika kiwanja cha Mpanda. Ujenzi wa "terminal building", miundombinu ya maji na ulinzi bado unaendelea; na

viii. Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mwl. Julius K. Nyerere umekamilika na mkandarasi wa ujenzi amepatikana na taratibu za kusaini mkataba zinaendelea.

### 2.4.6 Hali ya Hewa

Katika eneo hili, shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2012/13 ni: ununuzi wa vifaa na rada kwa ajili ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania; na kuwezesha vituo vya kutolea taarifa ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi kuwa na vifaa vya kisasa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kukamilika kwa tathmini ya *Geological survey* na ujenzi wa miundombinu ya rada katika Mkoa wa Mwanza unaendelea; kukamilika kwa ukarabati wa vituo vya kupokea mawasiliano ya hali ya hewa JNIA, Dodoma na Tabora; na taratibu za manunuzi ya vifaa vya hali ya hewa na CLIDATA zinaendelea.

### 2.4.7 Maendeleo ya Teknolojia na Ubunifu

Katika eneo hili, miradi itakayotekelezwa mwaka 2012/13 ni:

i. Kuendeleza ubunifu katika kuzalisha zana za kilimo zinazoendana na teknolojia ya kisasa kwa kuimarisha Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini. Hadi Desemba, 2012, *Centre For Agriculture Mechanization and Rural Technology* (CAMARTEC) imekamilisha kuunda kifaa cha kuchemsha maji kinachotumia mionzi ya jua na mashine ya kukata majani;

ii. Kuimarisha na kuendeleza uhandisi na usanifu katika ubunifu na uendelezaji wa mashine mbalimbali kwa ajili ya usindikaji mazao kwa

kuimarisha Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (Tanzania Engineering and Manufacturing, Designing Organisation). Utekelezaji ni: utengenezaji na majaribio ya mashine/vifaa kwa ajili ya machinjio ya kuku imekamilika; na ubunifu na utengenezaji wa kiteketezi cha taka za hospitali kisichotoa moshi mwingi na kisichotumia maji; na

iii. Kuimarisha taasisi za tathmini na ufuatiliaji wa viwango vya bidhaa vinavyohitajika katika soko hususan chakula kwa kuendeleza Taasisi ya Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni: uboreshaji wa majengo ya ofisi na maabara, kwa ajili ya uhakiki (Accreditation); na ununuzi wa vifaa muhimu kwa ajili ya uhakiki wa maabara za mazingira, kemia, chakula na vifaa vya kihandisi umekamilika.

### 2.4.8 Ardhi, Nyumba na Makazi

Katika mwaka 2012/13 kazi zilizopangwa ni pamoja na: kuendelea kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi, kuendelea na upimaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli za kiuchumi ikijumuisha uanzishwaji wa mji mpya wa Kigamboni; kuimarisha shughuli za utafiti na maendeleo ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Utekelezaji ni kama ifuatavyo:

i. Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uendelezaji na Ustawishaji wa Mji wa Kigamboni;
ii. Michoro ya kina inayoonyesha maeneo ya miundombinu ya barabara imeshaandaliwa. Michoro ya kina ya eneo la makazi mbadala katika mtaa wa Uvumba Kata ya Kibada imeandaliwa;
iii. Jumla ya vijiji 70 viliandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Mkoa wa Morogoro (Ulanga vijiji 15, Kilombero vijiji 46 na Tunduru vijiji 9); na
iv. Mafunzo juu ya sheria na uandaaji wa matumizi bora ya ardhi yalifanyika kwa watumishi wa Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi.

### 2.4.9 Utawala Bora

Katika mwaka 2012/13, shughuli zilizokusudiwa kutekelezwa ni: kuimarisha miundombinu na vitendea kazi kwa ajili ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; kujenga uwezo wa wataalam katika sekta ya sheria na kuongeza vitendea kazi; ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao na wawekezaji; na ujenzi wa miundombinu muhimu katika sekta ya sheria na utoaji haki. Utekelezaji ni: ujenzi wa majengo ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika miji ya Songea, Newala, na Tabora uko katika hatua za mwisho za kukamilika. Majengo katika wilaya za Kasulu na Mkinga yanaendelea vizuri na yatakamilika ifikapo Julai, 2013. Aidha,

mchakato wa kuwapata wajenzi wa majengo ya taasisi katika mikoa ya Mara, Mbeya, Kigoma na jengo la Umoja wa Afrika katika Mkoa wa Arusha unaendelea.

### 2.4.10 Katiba Mpya

Katika mwaka 2012/13, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilizunguka mikoa yote ya Tanzania (Bara na Visiwani) kukusanya maoni ya wananchi kuhusu uundwaji wa Katiba mpya. Bunge, Mahakama, Wizara, Taasisi na Idara zinazojitegemea na makundi maalum zilipata pia fursa ya kutoa maoni kuhusu Katiba Mpya. Kazi inayoendelea kwa sasa ni uundwaji wa mabaraza ya Katiba ili kujadili na kutoa maoni ya rasimu ya awali ya Katiba mpya.

### 2.4.11 Utambulisho wa Kitaifa

Katika mwaka 2012/13 hatua iliyofikiwa katika zoezi la kuandikisha raia ili kupata vitambulisho ni kama ifuatavyo: zoezi la utambuzi na usajili wa watumishi wa Serikali na Wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar limekamilika. Uhakiki wa taarifa na utoaji wa vitambulisho umeanza mwezi Februari, 2013 kwa viongozi mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Serikali. Vile vile, michoro ya Ofisi 40 za utambuzi na usajili za wilaya imekamilika na vitendea kazi kwa ajili ya zoezi la utambuzi na usajili vikiwemo kompyuta, kamera na *scanners* vimenunuliwa. Aidha, Makao Makuu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Dar es Salaam yamekarabatiwa na kuunganishwa na Mkongo wa Taifa.

### 2.4.12 Sensa ya Watu na Makazi 2012

Zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lilifanyika Agosti 2012 ili matokeo yake yatumike kupanga Mipango mbalimbali ya Maendeleo. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa Tanzania ina jumla ya watu 44,929,002 ambao kati ya hao 43,625,434 wako Tanzania Bara na 1,303,568 wako Zanzibar. Taarifa ya jumla inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2013. Aidha, Serikali inaendelea na uchambuzi wa taarifa za kina kuhusu jinsia na umri katika ngazi ya kitaifa, mikoa, wilaya na kata, pamoja na savei ya kuhakiki Sensa ya Watu na Makazi mwezi Mei, 2013 ili kufanya takwimu za Tanzania kukubalika kitaifa na kimataifa.

### 2.4.13 Mchango wa Sekta Binafsi

Katika kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi kama Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/13 ulivyolenga, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Katika kuongeza upatikanaji wa pembejeo nchini ikiwemo urahisi wa kupata mbolea, Kampuni ya YARA LTD imeanza ujenzi wa ghala la kuhifadhia

mbolea pembezoni mwa bandari ya Dar es Salaam. Ujenzi wa ghala hili unategemewa kukamilika Desemba, 2013 ambapo ghala litakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 45,000 kwa mara moja.

Sekta binafsi pia imetoa mchango mkubwa katika eneo la viwanda. Kampuni ya Athi River Mining (ARM) kutoka Kenya imejenga kiwanda eneo la Vikindu – Pwani chenye uwezo wa kuzalisha tani 800,000 za saruji kwa mwaka. Kiwanda hiki kimeanza kuzalisha na kuuza saruji chapa ya Rhino. Aidha kampuni hii inaendelea na ujenzi wa kiwanda kikubwa kipya Tanga, kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja na nusu kwa mwaka. Vilevile, maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha saruji huko Mtwara yameanza, ambapo kampuni ya Dangote Industries kutoka Nigeria tayari amepatiwa eneo la kujenga kiwanda hicho. Kwa upande wa mbolea, kampuni ya TATA chemicals ya India imeonesha nia ya kujenga kiwanda cha mbolea huko Mtwara. Maandalizi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi huo yameanza.

Kwa upande wa miundombinu makampuni mbalimbali yameshirikiana na Serikali katika kuendeleza miundombinu hususan kwenye reli, bandari na nishati. Hali kadhalika, katika eneo la utoaji wa huduma sekta binafsi imechangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza biashara, sekta ya fedha, utalii - ujenzi wa mahoteli, elimu – ujenzi wa shule na vyuo, afya-ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati.

## 2.5 Changamoto na Hatua Zilizochukuliwa

Katika utekelezaji wa bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/13, changamoto mbalimbali zilijitokeza. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Kukosekana au maandiko ya miradi kutokidhi vigezo vya kuwezesha upatikanaji wa mikopo hususan ile ya kibiashara;
ii. Ufinyu wa rasilimali fedha, upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa wakati, na baadhi ya wafadhili kutotimiza ahadi zao na kutozingatia mzunguko wa bajeti ya Serikali;
iii. Kukidhi matakwa ya utaratibu mpya wa kupata fedha za maendeleo kwa wakati, ikiwemo kuandaa taarifa za utekelezaji wa miradi kwa robo ya mwaka uliopita;
iv. Kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa robo ya kwanza kutokana na muswada wa fedha kupitishwa mwezi Agosti 2012;
v. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia sekta binafsi; na

vi. Uwezo wa kuajiri na kuvutia wataalam wenye ujuzi wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo.

Katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

i. Kuandaliwa kwa maelekezo ya uandaaji wa andiko la mradi na kuandaa mwongozo wa uwekezaji wa umma (Public Investment Manual);
ii. Kuendelea na juhudi za kuboresha upatikanaji wa mapato hususan mapato yasiyo ya kodi kwa kutumia mbinu mbalimbali na kuwahimiza wafadhili kutimiza ahadi zao na kuzingatia mzunguko wa bajeti;
iii. Kuboresha fomu za utoaji wa taarifa za miradi ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na mpango kazi na mtiririko wa mahitaji ya rasilimali fedha;
iv. Serikali imeridhia mabadiliko ya mzunguko wa bajeti, ambapo mkutano wa Bunge la bajeti utajadili bajeti ya Serikali 2013/14 kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2013. Mabadiliko haya yatawezesha utekelezaji wa bajeti ya 2013/14 kuanza mwezi Julai, 2013;
v. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini; na
vi. Kuendelea kuajiri, kuwavutia na kujenga uwezo wataalam wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo.

# SURA YA TATU

# MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2013/14

## 3.1 Utangulizi

Sura ya tatu inajumuisha maeneo yatakayopewa kipaumbele kwa mwaka 2013/14. Sura hii inajumuisha maeneo makuu mawili ambayo ni; maeneo ya kipaumbele ya kimkakati na maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Serikali itaendelea kutenga fedha kuendana na maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa pamoja na kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo iliyotekelezwa mwaka 2012/13.

## 3.2 Vigezo vya Kuainisha Miradi ya Kipaumbele ya Kimkakati

Miradi ya kitaifa ya kipaumbele kwa mwaka 2013/14 itazingatia vigezo vifuatavyo:

i. Matokeo ya haraka ya ukuaji uchumi, na kijamii ikiwa ni pamoja na kupunguza umaskini;
ii. Mchango kwa maendeleo ya maeneo mengine (multiplier effects);
iii. Kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi;
iv. Miradi inayogharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali na washirika wa maendeleo (counterpart funding projects), Mikataba na Hati ya Makubaliano (MoU);
v. Utoaji wa fursa za ajira na uwekezaji; na
vi. Miradi inayoendelea kutekelezwa.

## 3.3 Maeneo ya Kimkakati kwa mwaka 2013/14

Maeneo ya kimkakati yanajumuisha miradi mikubwa ambayo utekelezaji wake unaendelea pamoja na miradi ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi. Maeneo ambayo yatapewa kipaumbele kwa mwaka 2013/14 ni;

### 3.3.1 Miundombinu

**Usafiri na Usafirishaji**

**Reli**

i. Kuendelea kuimarisha Reli ya Kati kwa lengo la kuiongezea ufanisi;
ii. Kuendelea na ukarabati wa injini na mabehewa ya treni;
iii. Ununuzi wa injini pamoja na mabehewa mapya ya kubeba mizigo;
iv. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa njia mpya ya reli katika maeneo ya kimkakati;

v. Kuchangia katika miradi ya reli ya kikanda; na
vi. Kuboresha usafiri wa reli jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano wa abiria.

**Barabara**

i. Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa barabara zinazofungua maeneo yenye fursa za kiuchumi, kuunganisha Tanzania na nchi jirani, na kupunguza msongamano katika maeneo ya Mijini;
ii. Kuendelea na uboreshaji wa barabara zinazounganisha Mikoa na Wilaya; na
iii. Kuendelea na ujenzi wa Madaraja pamoja na Vivuko.

**Bandari**

i. Kuendelea na kuimarisha uboreshaji wa miundombinu ya bandari ili kuongeza uwezo wa kuhudumia mizigo kwa ufanisi;
ii. Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya; na
iii. Kuendelea na ujenzi wa mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi katika kujenga miundombinu na kuboresha usafirishaji wa mizigo.

**Uzalishaji na usambazaji wa umeme**

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme nchini;
ii. Kuendelea na ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Mtwara- Dar es Salaam, kituo cha kusafisha gesi, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji;
iii. Kuimarisha njia za usafirishaji na usambazaji wa umeme sambamba na kuhamasisha usambazaji wa umeme vijijini;
iv. Kuhamasisha uwekezaji katika kuzalisha umeme unaotokana na vyanzo vya nishati mbadala;
v. Kuandaa mpango kabambe wa matumizi ya gesi asilia nchini;
vi. Uanzishwaji wa hifadhi ya mafuta ya petroli nchini; na
vii. Kuboresha miongozo, sheria pamoja na taratibu zitakazosimamia matumizi ya gesi nchini.

**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

i. Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
ii. Kuanzisha maeneo maalumu ya TEHAMA;
iii. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa anwani za makazi na simbo za Posta;
iv. Kuendeleza miundombinu itakayoharakisha maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi; na

v. Kuhamasisha na kukuza tafiti za kimaendeleo.

**Maji Safi na Maji Taka**

i. Kuimarisha upatikanaji wa maji safi mijini na vijijini;
ii. Kuboresha miundombinu ya kusafirishia maji katika maeneo ya mijini na vijijini;
iii. Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji; na
iv. Kukarabati miundombinu ya maji taka mijini na vijijini.

### 3.3.2 Kilimo

i. Utekelezaji wa miradi ya miwa na mpunga katika maeneo ya mabonde ya Wami, Ruvu, Kagera, Kilombero na Malagarasi;
ii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya SAGCOT;
iii. Kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji;
iv. Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo, zana za kilimo pamoja na huduma za ugani (extension services);
v. Kuimarisha tafiti za kilimo;
vi. Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza katika kuongeza thamani mazao ya kilimo pamoja na upatikanaji wa masoko; na
vii. Kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula.

### 3.3.3 Viwanda

i. Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, hasa katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZ/SEZs);
ii. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini (Kurasini Logistical Trade Hub);
iii. Utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe Mchuchuma na chuma Liganga, pamoja na magadi katika Bonde la Engaruka na Ziwa Natron;
iv. Uendelezaji wa viwanda vinavyotumia rasilimali zinazopatikana hapa nchini kama vile usindikaji wa bidhaa za kilimo, nguo, makaa ya mawe, gesi asilia na chuma;
v. Kuendeleza miundombinu ya viwanda na kuboresha huduma za uwezeshaji;
vi. Kukuza na kuendeleza tafiti katika maeneo ya viwanda, uvumbuzi na maendeleo ya taasisi;
vii. Kukuza maendeleo ya wajasiriamali wadogo na wa kati kwa uanzishwaji wa maeneo maalum ya viwanda;
viii. Kuendelea kuimarisha viwanda vidogo chini ya SIDO; na
ix. Uhaulishaji wa teknolojia ya uzalishaji matrekta na zana za kilimo.

### 3.3.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu

Kuimarisha uwezo wa kila sekta kufanya mipango halisi ya rasilimali watu, maendeleo ya rasilimali watu na kuchambua mahitaji ya ujuzi. Aidha, mkazo utawekwa katika kutoa mafunzo katika maeneo mahsusi (targeted training in specialized fields) hasa kwa wataalam wa gesi na mafuta, chuma, urani, madini na umwagiliaji na maji.

### 3.3.5 Utalii na Huduma za Fedha

**Utalii**

i. Kujenga na kuboresha vivutio vya utalii nchini;
ii. Kuwezesha vivutio vya utalii kufikika kwa kujenga miundombinu ya barabara pamoja na kuboresha viwanja vya ndege;
iii. Kuimarisha ushiriki wa jamii katika usimamizi wa hifadhi ya wanyamapori na rasilimali zitokanazo na urithi wa kitamaduni; na
iv. Kuongeza na kupanua vivutio pamoja na bidhaa za utalii.

### 3.3.6 Huduma za kifedha

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibenki na fedha;
ii. Kuanzisha na kuimarisha maendeleo ya taasisi za fedha; na
iii. Kuimarisha huduma za upatikanaji mikopo.

## 3.4 Maeneo Mengine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi

Pamoja na kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kitaifa kwa mwaka 2013/14, maeneo mengine ambayo miradi itaibuliwa na sekta /mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa na kutekelezwa katika ngazi hiyo ni;

### 3.4.1 Elimu / Mafunzo ya Ufundi

i. Kuimarisha upatikanaji wa elimu bora katika taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi kwa kuhakikisha uwepo wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, maktaba, maabara na vyumba vya mihadhara;
ii. Kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari;
iii. Kuimarisha mfumo wa kugharamia elimu ya juu / mfumo wa mikopo ya elimu ya juu; na
iv. Kutekeleza programu ya pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo "*Education Reform Compact* (ERC)" katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu Nchini ili kufikia malengo ya milenia.

### 3.4.2 Afya na Ustawi wa Jamii

i. Kuimarisha ubora na upatikanaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii kwa kuhakikisha upatikanaji wa madawa na vifaa tiba, kuimarisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya na hospital za rufaa;
ii. Kuimarisha utekelezaji wa mpango wa uboreshaji wa sekta ya afya, usimamizi na kupunguza vifo vya wajawazito;
iii. Kuimarisha tiba, matunzo na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyo ya kuambukiza na magonjwa ya kitropiki; na
iv. Kuboresha upatikanaji wa rasilimali watu katika sekta ya afya kwa kuimarisha taasisi za mafunzo.

### 3.4.3 Mifugo na Uvuvi

i. Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo kama vile malisho, majosho, na malambo;
ii. Kukuza huduma na uzalishaji wa samaki;
iii. Kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa kwa ajili ya maendeleo ya mifugo na uvuvi,
iv. Kuimarisha taasisi zinazoshughulikia tafiti, na
v. Kuongeza thamani mazao ya mifugo na uvuvi.

### 3.4.4 Misitu na Wanyamapori

i. Kuimarisha shughuli mbalimbali za usimamizi wa ufugaji nyuki, misitu na wanyamapori;
ii. Kuhamasisha uwekezaji katika shughuli za kuongeza thamani mazao ya nyuki, wanyamapori na misitu;
iii. Kuendelea kujenga uwezo wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi wa hewa ukaa;
iv. Kuwezesha wananchi na sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza na kusimamia misitu, nyuki na wanyama pori; na
v. Kuongeza upatikanaji na matumizi ya vifaa bora vya kisasa kwa ufugaji nyuki.

### 3.4.5 Madini

i. Uendelezaji wa shughuli za kuongeza thamani ya madini;
ii. Kuendeleza taarifa za kisayansi kuhusu madini;
iii. Kuendeleza miundombinu katika taasisi za Geological Survey of Tanzania (GST), Mineral Research Institute (MRI) na Tanzania Mineral Auditing Agency (TMAA)/TANSORT;
iv. Kuendeleza sekta ya wachimbaji wadogo wa madini;
v. Utekelezaji wa mradi wa usimamizi rasilimali endelevu wa madini;

vi. Kuboresha upatikanaji wa zana na vifaa vya madini kwa wachimbaji wadogo, na
vii. Kuimarisha tafiti, utafutaji na uwezo wa kusimamia madini.

### 3.4.6 Ardhi, Nyumba na Makazi

i. Kuendelea kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi;
ii. Kuendelea na upimaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli za kiuchumi ikijumuisha uanzishwaji wa mji mpya wa Kigamboni; na
iii. Kuimarisha shughuli za utafiti na maendeleo ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

### 3.4.7 Usafiri wa Anga

i. Kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuongeza uwezo wa kusafirisha abiria na mizigo;
ii. Kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege katika maeneo ya kimkakati na kukarabati vilivyopo; na
iii. Kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha sekta binafsi kuwekeza katika usafiri wa Anga.

### 3.4.8 Hali ya Hewa

i. Kuinua uwezo wa kitaasisi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na
ii. Kuimarisha shughuli za utabiri wa hali ya hewa ikihusisha ufungaji wa vifaa vya kisasa katika Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kusambaza vifaa hivyo kwenye vituo vya taarifa vya hali ya hewa.

### 3.4.9 Biashara na Masoko

i. Kuendelea kujenga na kuendeleza miundombinu ya masoko ikijumuisha kuanzisha mfumo mpana wa taarifa za masoko na biashara (intergrated marketing information system); na
ii. Kuanzisha soko la mazao na bidhaa *(Commodity Exchange).*

### 3.4.10 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

i. Kuimarisha utekelezaji wa Umoja wa Forodha ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikijumuisha kukamilisha ujenzi wa vituo vya utoaji huduma za pamoja mipakani (OSBP);
ii. Kuandaa Mpango wa utekelezaji wa miradi ya vipaumbele vya miundombinu ya Kanda ya Afrika Mashariki;
iii. Kufanya mapitio, tathmini na tafiti kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji wa mtangamano wa Afrika Mahariki pamoja na kutoa elimu juu ya fursa zilizopo;

iv. Kuimarisha uwezo wa kitaasisi kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mtangamano kikanda na ushirikiano wa kimataifa; na
v. Kuendelea kutekeleza mkakati wa Taifa wa soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 3.4.11 Utambulisho wa Kitaifa

Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya Taifa.

### 3.4.12 Utawala Bora

i. Kutekeleza Mpango kazi wa kitaifa wa kujitathmini katika masuala ya utawala bora *(African Peer Review Mechanism-National Plan of Action –APRM- NPoA)*;
ii. Kutekeleza mpango kazi wa kitaifa wa utawala bora na haki za binadamu; na
iii. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya sekta ya sheria, usalama wa raia na utawala bora.

### 3.4.13 Katiba Mpya

Kuendelea na mchakato wa uundaji wa Katiba mpya.

### 3.4.14 Kazi na Ajira

i. Kuendelea kuwezesha miradi midogo kwa ajili ya mifuko na mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana, wanawake na makundi maalum;
ii. Programu za kukuza ajira, maendeleo na haki ya mtoto;
iii. Kuimarisha mfumo wa usimamizi, ukaguzi, usuluhishi na uamuzi wa migogoro sehemu za kazi; na
iv. Kuimarisha mifumo na udhibiti wa hifadhi ya jamii.

# SURA YA NNE

# UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA

## 4.0 Utangulizi

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo 2013/14 kwa ufanisi hapana budi kuwa na vyanzo vya mapato vyenye uhakika ili kuweza kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Vyanzo hivyo vitatokana na mapato ya ndani, misaada, mikopo pamoja na ushiriki wa sekta binafsi.

## 4.1 Gharama za Kutekeleza Mpango

Katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Serikali italazimika kutenga rasilimali za kutosha kila mwaka kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Katika kugharamia mpango wa maendeleo wa miaka mitano ilikadiriwa kuwa shilingi trilioni 8.9 zitahitajika kila mwaka, kati ya hizo shilingi trilioni 2.9 zitatokana na fedha za ndani katika bajeti ya Serikali na shilingi trilioni 6.0 zitatokana na uwekezaji wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Jambo muhimu la kusisitiza ni kuwa rasilimali chache zilizopo ni lazima zitumike katika kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi na ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

## 4.2 Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Serikali itaendelea kutumia vyanzo vya ndani vya mapato vilivyopo pamoja na kubuni vyanzo vipya vya kugharamia Mpango wa Maendeleo 2013/14. Aidha, Serikali inatarajia kukopa ndani ya nchi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Serikali itaendelea kuzingatia sera ya kukopa ndani ya nchi isiyozidi asilimia moja ya Pato la Taifa, ambapo mikopo hiyo itaelekezwa kwa mashirika ya umma na benki za kibiashara kupitia uuzaji wa dhamana za Serikali.

## 4.3 Vyanzo vya Mapato ya Nje

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo 2013/14, vyanzo vya mapato ya nje vitatokana na misaada, ikijumuisha ruzuku na mikopo yenye masharti nafuu. Vilevile, Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka kwa nchi marafiki na mashirika ya kimataifa kwa kuzingatia uhimilivu wa deni la Taifa. Aidha, katika kupunguza nakisi ya bajeti ya ugharamiaji wa kutekeleza Mpango wa Maendeleo 2013/14, Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na nchi wahisani na mashirika ya kimataifa ili kuweza kusaidia utekelezaji wa Mpango.

### 4.4 Kukuza Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Serikali itaendelea kutumia mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan, miradi ya miundombinu. Serikali imekamilisha taratibu za kisheria katika eneo hili ikiwa ni pamoja na sera, sheria na kanuni zake. Elimu itaendelea kutolewa kwa wadau wa sekta binafsi ili washiriki kikamilifu katika uwekezaji kwa ubia na sekta ya umma.

### 4.5 Kuvutia Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Serikali inaendelea kutambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa, hivyo kipaumbele kitawekwa katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji iii kuvutia uwekezaji mkubwa wa sekta binafsi katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Aidha, sekta binafsi itaendelea kuhamasishwa kuendelea kuchangia shughuli za maendeleo ili kupunguza mzigo katika bajeti ya Serikali.

# SURA YA TANO

# UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MPANGO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua kwa muhtasari mfumo wa utekelezaji wa mapendekezo ya mpango wa maendeleo kwa mwaka 2013/14, ikibainisha shughuli zinazopaswa kufanyika katika utayarishaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango.

## 5.1 Mpangilio wa Utekelezaji

**Utayarishaji na uidhinishaji wa Mpango wa Mwaka**

Kila Wizara, Idara zinazojitegemea na wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuandaa mipango ambayo itaonyesha kwa ufasaha gharama za uwekezaji (Capital Investment) na kiutawala. Aidha, miradi itakayoainishwa itofautishe ile ya kimkakati na miradi mingine kwa ukuaji wa uchumi. Vile vile, kipaumbele kiwe ni miradi yenye kuleta matokeo ya haraka hususan katika kuchochea maendeleo ya maeneo mengine na program nyingine katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Ili kuboresha utekelezaji wa mpango kwa ufanisi zaidi, ushirikishwaji wa umma ni muhimu. Katika kuushirikisha umma katika kupanga mipango ya maendeleo, kunatakiwa kuwepo na mfumo wa vikao vya mipango vitakavyoanzia katika ngazi za chini kabisa za utendaji. Mipango ya Mikoa itaanzia na vikao vya ngazi ya vijiji, kata, halmashauri za wilaya, na hatimaye ngazi ya mkoa. Mpango uliopitishwa na Mkoa utawasilishwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Hivyo hivyo itakuwa kwa Wakala za Serikali nazo zitatayarisha mipango yao ya mwaka na kuiwasilisha kwa Wizara husika. Katika ngazi ya Wizara kutakuwepo na vikao vya wizara ambavyo vitachambua na kukamilisha mipango ya sekta husika. Rasimu ya Mpango iliyopitishwa na Wizara itawasilishwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango.

## 5.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Katika hatua za awali za kufanya ufuatiliaji na tathmini, Tume ya Mipango ilifanya uchambuzi wa Mipango Kazi na mtiririko wa mahitaji ya fedha ya Miradi ya Maendeleo kwa wizara na taasisi. Uchambuzi huo unafanyika katika kila robo mwaka, ukizingatia Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12-2025/26), Mpango wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/13.

Vigezo vilivyotumika katika uchambuzi huo ni: (i) Mpango Kazi *(Action Plan)*

wenye vigezo mahsusi vya kupima matokeo ya utekelezaji; (ii) Mtiririko wa mahitaji ya Fedha *(Cash flow Plan)* unaendana na mpango-kazi kwa kila robo mwaka; (iii) Fedha zinazoombwa za miradi ya maendeleo 2012/13 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo 2012/13 (Vol. IV); (iv) Jina na namba za miradi kama zinavyoonekana katika kitabu cha bajeti ya maendeleo 2012/13 (Vol. IV); (v) Mchanganuo wa bajeti ya mahitaji ya fedha za ndani na nje kwa kila mradi; (vi) Uzito uliowekwa kwenye miradi ya kitaifa ya kimkakati ikilinganishwa na miradi mingine kwa kila Fungu; (vii) Uzito uliowekwa kwenye shughuli za kuongeza uzalishaji *(capital investment)* ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo yenye sura ya matumizi ya kawaida ya kiuendeshaji; (viii) Kuwepo hati za madai na taarifa za utekelezaji kwa miradi inayotekelezwa na Makandarasi au Mtaalam Mwelekezi; Kuwepo hati ya malipo ya fidia na ratiba ya kulipa *(compensation schedule)* kwa miradi inayojumuisha ulipaji fidia; (ix) Kiasi kinachohitajika kwa ajili ya mchango wa Serikali *(counterpart funds)*, na mahitaji ya kimkataba au hati ya makubaliano (MOU); (x) Andiko la mradi kwa miradi mipya: aina ya mradi, kipindi cha utekelezaji wa mradi, ugharamiaji wa mradi na faida kwa Taifa; na (xi) Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya zamani inayoendelea: aina ya miradi, kipindi na hatua za utekelezaji, changamoto za utekelezaji na mkakati wa kukamilisha mradi.

Taarifa ya uchambuzi wa mipango kazi hiyo iliwasilishwa na kujadiliwa katika semina ya kazi *(retreat)* ya Baraza la Mawaziri mwezi Oktoba, 2012. Matokeo ya uchambuzi huo yalibaini kuwa: (i) Wizara, Idara na Wakala wa Serikali nyingi zimeanza kuandaa andiko la mradi *(project write-ups)* kuonesha shughuli zinazopangwa kutekelezwa, makadirio ya gharama husika na vigezo mahsusi vya kupima mafanikio ya utekelezaji; (ii) mapendekezo ya bajeti za maendeleo kwa sehemu kubwa yamezingatia yalihusu gharama halisi *capital investment* badala zile za kiutawala; na (iv) kuzingatia Mwongozo wa Mpango na Bajeti ipasavyo wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali/ Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuwa na utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kuwa mipango-kazi, maoteo ya mahitaji ya fedha *(cash flow plans)* na MTEFs zinazingatia makubaliano yaliyofikiwa wakati wa uchambuzi wa bajeti *(budget scrutinisation)*.

Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ilifanya ufuatiliaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo mwezi Februari 2013 katika sekta za miundombinu, nishati, kilimo, maji, viwanda na elimu. Lengo la ufuatiliaji huo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa hatua za utekelezaji wa miradi zinaendana na mpango kazi na fedha zilizotolewa kwa kipindi cha nusu mwaka 2012/13. Tathmini ya awali inaonesha kuwa miradi mingi ipo nyuma ya ratiba kutokana na changamoto

mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha, taratibu za manunuzi na madeni ya miaka iliyopita. Aidha, kutokamilika kwa tathmini ya fidia, uhakiki na ulipaji wa fidia kwa wakati imechangia baadhi ya miradi kutotekelezwa kwa wakati. Vilevile, miundombinu na huduma wezeshi hususan barabara, maji na umeme ni changamoto kwa baadhi ya miradi kutekelezwa kwa wakati. Mpango wa mwaka 2013/14, pamoja na mambo mengine umelenga kutatua changamoto hizi.

### 5.3 Utaratibu wa Kusimamia Fedha za Maendeleo

Katika kuhakikisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zinalindwa na zinatumika katika shughuli zilizopangwa, utaratibu uliowekwa ni kama ifuatavyo:

i. Wizara, Idara na Wakala/Taasisi za Serikali kuwasilisha Mpango Kazi na Mtiririko wa mahitaji ya rasilimali fedha Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na nakala kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Wizara ya Fedha mara baada ya bajeti zao kuidhinishwa na Bunge;
ii. Wizara, Idara na Wakala/Taasisi za Serikali kujaza Fomu TFN 358 kwa miradi iliyopata idhini ya Tume ya Mipango na kuwasilisha Wizara ya Fedha. Tume ya Mipango itapatiwa nakala ya mwisho ya fomu hiyo na Wizara ya Fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini;
iii. Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zitatakiwa kuwasilisha Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha taarifa ya kila robo mwaka si zaidi ya wiki mbili baada ya robo mwaka unaotolewa taarifa husika kwa uchambuzi. Taarifa hizo ziambatane na taarifa ya Mkaguzi wa ndani wa Wizara/Taasisi; na
iv. Fedha za robo mwaka inayofuata zitatolewa tu pale ambapo Tume ya Mipango itaridhika na taarifa ya utekelezaji wa robo iliyopita.

### 5.4 Mfumo wa Kusimamia Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini kwa Miradi ya Maendeleo

Serikali imefanya maamuzi ya kuanzisha mfumo mpya wa kusimamia utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo hapa nchini kwa kutumia uzoefu wa nchi ya Malaysia kupitia *Performance Management and Delivery Unit* (PEMANDU). Mfumo huu utajumuisha uanzishwaji wa taasisi itakayofanya kazi hiyo ya ufuatiliaji katika kutanzua matatizo na changamoto za kiutendaji zitakazokuwa zikikabili sekta zinazohusika na utekelezaji wa miradi ya maendeleo - *President's Delivery Bureau (PDB)*. Aidha, mfumo huu utajumuisha uchambuzi wa kina wa kimaabara (*labs*) unaolenga kuandaa programu za utekelezaji za miradi ya maendeleo zilizochanganuliwa kwa kina (*detailed program*), vigezo vya kupima utekelezaji (*key performance*

*indicators*) na vya kufanya ufuatiliaji na tathmini (tools for monitoring and evaluation).

Utekelezaji wa *labs* umeanza kwa kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 22 Februari, 2013 na unaendelea hadi tarehe 4 Aprili, 2013. Kwa kuanzia maeneo ya yanayofanyiwa uchambuzi kwa kutumia utaratibu wa huu ni:

i. **Nishati ikijumuisha mafuta na gesi**: Kuzalisha Megawati 2780 za umeme kufikia mwaka 2015 na kuhakikisha mafuta na gesi vinatumika kwa manufaa ya nchi na watu wake ;
ii. **Uchukuzi**: Kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji kwa kufungulia ukanda wa kati (Central Transport Corridor) kwa kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es salaam na kukarabati reli ya kati;
iii. **Mapato**: Kuongeza mapato ya Serikali kwa asilimia 50 kwa kutumia vyanzo vipya kutoka ndani na nje ya nchi;
iv. **Kilimo**: Kuhakikisha Sekta hii inakua kwa asilimia 6 kwa mwaka kwa kuongeza tija na thamani, kutoa ajira zisizopungua 200,000 na kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada nje ya nchi;
v. **Elimu**: Kuongeza ubora wa elimu mara mbili kutoka kiwango cha sasa na kuongeza ujuzi utakaosaidia kuharakisha maendeleo ya viwanda; na
vi. **Maji**: kuimarisha huduma za maji mijini na vijijini.

### 5.5 Muhtasari wa Uratibu wa Utekelezaji

Jedwali na 1. Linaelezea muhtasari wa ratiba ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utayarishaji mapendekezo ya mpango, na pia taasisi zitakazohusika kwa kila shughuli.

**Jedwali Na 1: Ratiba ya uandaaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2013/14**

| Shughuli | Muda | Mamlaka Husika |
|---|---|---|
| Kuanza Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | Agosti, 2012 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango |
| Kuandaa Rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka | Agosti 2012 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango |
| Kuwasilisha rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka kwa wadau mbalimbali | Septemba 2012 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Wizara, Idara ,Mashirika / Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi |
| Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele | Oktoba 2012 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango |
| Kupitia rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka kwa wadau mbalimbali | Novemba 2012 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Wizara, Idara ,Mashirika / Serikali za Mitaa |
| Kuwasilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo Baraza la Mawaziri | Desemba 2012 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango |
| Kuwasilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo katika Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi | Januari 2013 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango |
| Kuwasilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo Bungeni | Februari 2013 | Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango |

Kimepigwa chapa na kiwanda cha Uchapaji, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Press "A"
S.L.P 9121, Simu: +255 22 2110692, Barabara ya Magogoni, DAR ES SALAAM.